MAHAKAMA YA KIMATAIFA YA JINAI (ICC-THE HAGUE)

UFAFANUZI WA VIFUPISHO

ICC - Mahakama ya Kimataifa ya jinai (International Criminal Court)

ICTR - Mahakama ya Kimataifa ya jinai ya Rwanda (International Criminal Tribunal for Rwanda)

ICTY - Mahakama ya Kimataifa ya jinai ya Yugoslavia ya zamani International Criminal Tribunal for the Former Yugoslavia.

SCSL - Mahakama maalumu ya Siera Leone (Special Court for Siera Leone)

STL - Mahakama maalumu ya Lebanon (Special Tribunal for Lebanon)

ECCC - Kitengo kisicho cha kawaida katika Mahakama za Kambodia (Extraordinary Chambers in the Courts of Cambodia).

UN - Umoja wa Mataifa (United Nations)

ICJ - Mahakama ya Kimataifa ya Haki (International Court of Justice)

RPF - Rwanda Patriotic Front

*RTLM - **Radio-Télévision Libre des Milles Collines**.*

CDR - Coalition for the Defence of the Republic.

JIFUNZE SHERIA
LAW BOOKS & CASE LAWS

YALIYOMO

(1) Kuhusu Mwandishi.....5

(2) Dibaji.....6

(3) Mahakama ya ICC ni nini?.....7

(4) Mahakama ya ICC iliundwa lini?.....7

(5) Makosa yanayoshughulikiwa na ICC.....7

(6) Makosa ya ICC yanatambulikaje na sheria za Tanzania.....8

(7) Makao makuu ya ICC yako wapi?.....9

(8) Mamlaka ya ICC ni ya namna gani?.....9

(9) Wanachama wa ICC.....10

(10) Utofauti kati ya ICC na Mahakama nyingine za kimataifa.....12

(11) Utofauti wa ICC na ICJ.....12

(12) Mahusiano ya ICC na Umoja wa Mataifa (UN).....13

(13) ICC ni mbadala wa Mahakama zetu?.....13

(14) Mazingira yanayoifanya ICC isiwe na mamlaka.....14

(15) Maana ya kutokuwa na nia ya kushitaki.....15

(16) Maana ya nchi kutokuwa na uwezo kushitaki.....16

(17) Aina ya watu wanaoweza kushitakiwa ICC.....16

(18) Nani anaweza kukwepa kushitakiwa ICC.....17

(19) Namna mashitaka yanavyoanzishwa kule ICC.....18

(20) Mwendesha Mashitaka kuanzisha mchakato mwenyewe.....19

(21) Nchi Mwanachama ikipeleka ombi ICC kuanzisha mchakato.....20

(22) Nchi Mwanachama ambao walishapeleka maombi ICC.....20

(23) Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupeleka Maombi.....22

(24) Nini hutokea ombi lenye tuhuma likifikishwa ICC.....22

(25) Kama kosa la jinai linaweza kupitwa na wakati.....22

(26) Nani ana uweza kushitakiwa ICC?.....23

(27) Hatua kwa hatua za mwenendo wa shitaka.....23

(28) Uthibitishwaji kama kuna kosa la msingi.....25

(29) Usikilizwaji kamili wa kesi.....27

(30) Makosa ya kimbari.....28

(31) Makosa ya Uhalifu dhidi ya Ubinadamu.....31

(32) Makosa ya Kivita.....36

(33) Makosa ya uchokozi wan chi.....42

(34) Namna chuki zinavyoweza kusambazwa na kuleta tatizo.....44

(35) Funzo kwa yaliyotokea Rwanda mwaka 1994.....44

(a) Chuki na uadui zilivyotokea.....45

(b) Kuwafananisha Watutsi na wadudu.....46

(c) Propaganda za vitisho kwa wananchi.....47

(d) Wachora vikatuni.....47

(e) Uhusika wa viongozi na watu mashuhuri.....47

(f) Matumizi ya misamiati, nahau na mafumbo.....48

(g) Mwanasiasa Jean Paul Akayesu.....49

(h) Waziri Mkuu Jean Kabanda.....50

(36) Matumizi mabaya ya vyombo vya habari.....50

(37) Uhusika wa wanamuziki katika jamii.....54

(38) Uhusika wa Makanisa.....55

(39) Kiongozi kuwajibishwa kwa makosa ya walio chini yake.....56

(40) Machafuko Lebanon.....58

(41) Funzo toka uchaguzi wa Kenya mwaka 2007/2008.....60

(42) Vikundi vya ulinzi kwenye vyama vya siasa Tanzania.....61

JIFUNZE SHERIA
AW BOOKS & CASE LAW

KUHUSU MWANDISHI

Ofmedy Mussa Mtenga alizaliwa Wilaya ya Kilolo Mkoa wa Iringa miaka 40 iliyopita na amekuwa Mwendesha Mashitaka wa Jamhuri kwa miaka 9 mfululizo, tangu Februari 2011 hadi sasa. Kwa sasa ni Wakili wa Serikali katika ***Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (Ofisi ya DPP)*** Mkoa wa Mbeya.

Alipata Shahada ya kwanza ya Sheria (L.L.B) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 2007 na Shahada ya Uzamili ya Sheria za jinai za Kimataifa (***L.L.M in International Crime and Justice***) katika Chuo Kikuu cha Torino(Turin) Italia katika kituo kikuu cha mafunzo cha Umoja wa Mataifa (UN training centre) kitengo cha Taasisi ya utafiti wa Makosa ya Jinai za Kimataifa na jinai zinazovuka mipaka (UNICRI - United Nations Interregional Crime and Justice Research Institute (UNICRI) mwaka 2009/2010. Taasisi hii imejikita zaidi katika utafiti wa *makosa ya jinai ya kimataifa na mashitaka yake ICC, ICTR, ICTY na Mahakama za mchanganyiko, na* ***makosa yanayovuka mipaka*** *kama* ***usafirishaji madawa ya kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, fedha haramu, nyara, utakatishaji fedha*** *na makosa yanayofanana na hayo*. Mwaka 2013 akiwa anaendelea kufanya kazi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alifaulu mtihani wa Uwakili (Bar Examination) na kuthibitishwa kuwa wakili wa Mahakama Kuu na Mahakama za chini yake.

Ofmedy ni Wakili aliyepata uzoefu na ubora haraka kutokana na tabia kusoma kwa kufanya tafiti na kuandika vitabu na ameendesha kesi Mahakama ya Rufaa ya Tanzania tangu 2016 hadi leo. Zipo kesi nyingi sana ameiwakilisha Serikali, baadhi zimejumuishwa kwenye vitabu vyake ambavyo kila aliyevipata amevisifia kuwa ni vya msaada Mahakamani.

Unashauriwa utafute bila kukosa vitabu vyake ambavyo vimekuwa msaada mkubwa sana kwa ***Mawakili wa Serikali*** na ***wa Kujitegemea, Waheshimiwa Mahakimu*** na ***Wah. Majaji*** katika kuendesha mashauri ya jinai kwa Mahakama zote nchini hadi Mahakama ya Rufaa. Vitabu hivyo ni "***Criminal Practice Manual, A step by step guide to Trials in Subordinate Courts***", na "***Criminal Practice Manual , A best Practice Guide to Trials in the High Court***" na vya kiswahili vinavyolenga raia wa kawaida ni kama "**Haki ya Kupata Dhamana Polisi na Mahakamani**" na mwaka 2013 aliwahi kuandika kitabu cha "**Taratibu za kugawamirathi na Wosia**" Mwaka huu 2020 pia anatoa kitabu cha "**Appeals and Applications before the Court of Appeal of Tanzania**" kinachoongelea ***aplications, appeals, Review na References***.

Muda wote siku zisizo za kazi kama wikendi, sikukuu, na majira ya usiku, **Ofmedy** hutumia kujisomea na kuandika vitabu, ambavyo pia vimemuimarisha katika kuendesha kesi Mahakamani kwasababu yote yaliyopo kwenye vitabu vyake, yapo kichwani kwake jambo lililomfanya awe bora katika kesi za jinai akiwa Mahakamani.

Kuona vitabu pitia**www.sheriakwakiswahili.blogspot.com**
Kwa vitabu mbalimbali piga **0767154141**

DIBAJI

Katika makala hii nimechagua vitu vichache, vile vya msingi tu kumwezesha msomaji wa kawaida kufahamu maana, makosa na jinsi ICC inavyofanya kazi. Ningeandika kiundani zingekuwepo kurasa nyingi zenye kuchosha msomaji, wakati lengo lilikuwa kupeleka ufafanuzi mwepesi na wa moja kwa moja kwa wasomaji ambao wengine ni raia wa kawaida kabisa au wengine pengine hawana kiwango cha juu cha elimu. Sheria za jinai za kimataifa na taratibu za kuendesha mashauri yake ni pana na zingechukua kitabu kikubwa sana. Lengo ni kuifanya jamii kuifahamu ICC na makosa inayoyashughulikia ili wasiyatende. Pia, watu wengi wanafikiri kila kosa linaweza kushughulikiwa na ICC kama vile ICC ni mbadala wa mahakama zetu nchini. Makala hii itajibu maswali hayo. Pia msomaji utaweza kutambua kama ICC ni ya muhimu au la.

Maadamu Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizotia saini ***Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya jinai wa 1998***, tunawajibika na Mahakama hii. Na hata kama tusingekuwa tumesaini au tungekuwa tumejitoa baada ya kusaini, bado isingekuwa kinga ya moja kwa moja kwa watuhumiwa kuepuka mashitaka yake yote.

Makala hii haijaandikwa kwa shinikizo au kuegemea upande wowote, iwe wa vyama vya siasa, makundi ya kidini, Serikali au kikundi chochote cha aina yeyote ndani au nje ya Tanzania. Pia haijaandikwa ikilenga kukosoa chochote nchini au katika nchi yeyote Africa, imeandikwa kwa nia njema kabisa ya kusambaza uelewa kwa jamii, nikijua kwa namna moja au nyingine kuna kitu Watanzania wataokota kitakachokuwa cha manufaa kwao na kwa nchi. Makosa yanayoendeshwa na ICC yote ni yale mazito na yanahusisha machafuko, tukiyaelewa na kusaidiana kuzuia vyanzo vyake itatunufaisha kama nchi kulinda amani, mshikamano na ustawi.

Kutokana na tunayoyaona yakiendelea duniani, maandamano katika nchi mbalimbali, wananchi kukabiliana na polisi kwa namna mbalimbali, uasi katika nchi mbalimbali barani Afrika, mapigano ya kidini Jamhuri ya Afrika ya kati na Naijeria, mapigano ya kisiasa, vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyotokea nchi za maziwa makuu miaka ya Tisini, vikundi vya kigaidi, mapigano Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mauaji ya kimbari Rwanda 1994, uenezaji wa moja kwa moja wa chuki kwa njia ya mitandao ya kijamii, matumizi mabaya ya vyombo vya habari kama magazeti na redio, matumizi mabaya ya nyumba za ibada kwa mahubiri yenye chuki dhidi ya dini zingine au Serikali hata kupelekea baadhi ya vyombo kufungiwa n.k. ni muhimu watu wakajua matokeo ya yale wanayoyatenda endapo yatasababisha madhara yanayoangukia kwenye makossa yanayoendeshwa na ICC, pengine kwa kujua huko tunaweza kuyaepuka kabla hayajatokia. Tumejifunza pia matokeo ya fujo za baada ya **uchaguzi Kenya mwaka2007/2008** jinsi zilivyoleta usumbufu kwa wanasiasa na waandishi wa habari.

Tafadhali, naomba jitahidi kusoma nakala hii yote, usiishie njiani!

Mahakama ya ICC ni nini?

Mahakama ya Kimataifa ya jinai (ICC), ni Mahakama ya kimataifa ya kudumu, iliyoundwa kupeleleza, kushitaki na kuendesha mashitaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa yanayoangaliwa kama ndio mazito kupindukia katika jumuiya ya kimataifa. Hii ina maana kwamba, pamoja na kwamba katika jumuiya ya kimataifa yapo makosa mengi, yalichaguliwa yale yanayotazamwa kama ndio mazito kupindukia yanayohitaji jicho la tofauti na kushughulikiwa kimataifa. Makosa hayo ni haya yafuatayo: **-**

1. Makosa ya Kimbari
2. Uhalifu dhidi ya ubinadamu
3. Makosa ya kivita
4. Kosa la Uchokozi kwa nchi

Ni Makosa haya manne tu ndiyo jumuiya ya Kimataifa iliyaona ni mazito na ya kutisha kuliko mengine na maalumu yanayotakiwa kushughulikiwa kimataifa katika Mahakama hii. Makosa mengine yote hata kama yatahusisha mauaji, mateso n.k, kwasababu hayagusi viini vya makosa tajwa hapo juu, ICC haina mamlaka kuyashughulikia, zimeachiwa nchi husika kushughulikia kwa kutumia mifumo ya utoaji haki katika nchi zao. Vilevile, walengwa katika makosa hayo sio kila aliyetenda kosa, bali wahusika wakuu pekee.

Mahakama ya ICC iliundwa lini?

Kuundwa kwa ICC kulianza mwaka 1998 kwa mkataba ujulikanao kama "**Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya jinai"** ambao ulianza kufanya kazi tarehe ***01 Julai, 2002***. Nchi zilizotia saini kukubaliana uanachama wa mkataba wa Roma ndio nchi wanachama wa ICC. Zipo nchi ambazo hazijatia saini mkataba huu kuwa wanachama lakini zimekubali kutoa ushirikiano panapohitajika, kwa namna ya kuchangia michango ya kuendesha Mahakama, kukamata watuhumia na kadhalika.

Makosa gani ICC inashughulikia?

Kwa ufafanuzi zaidi, nitarudia kuyataja makosa ambayo ICC inayo mamlaka kushughulikia. Ni makosa manne (4) tu ambayo ni: -

(1) Makosa ya Kimbari (Genocide)

(2) Uhalifu dhidi ya ubinadamu (Crimes against Humanity)

(3) Makosa ya kivita (War Crimes)

(4) Kosa la uchokozi kwa nchi (Crime of aggression).

Kila kosa tajwa hapo juu linavyo viini vyake na Mwendesha Mashitaka anapoanzisha mchakato lazima ajihakikishe mazingira yanaonyesha vitendo vyenye viini vya makosa hayo vimetendeka. Kesi haitaruhusiwa kuendelea na usikilizwaji kamili bila shauri la kuthibitisha mashitaka (***confirmation of charges***), na kama viini hivyo havipo usikilizwaji kamili hautaruhusiwa.

Makosa hayo kwa Sheria za Tanzania yanachukuliwaje?

Tanzania katika sheria zake haijaasili viini vya makosa hayo moja kwa moja kama yanavyoainishwa katika Sheria ya Mahakama ya ICC (*ICC Statute*). Hata hivyo, labda kutokana na uzoefu tuliokutana nao toka nchi za maziwa makuu zinazotuzunguka, sheria zetu kwa mbali zimeanza kuakisi ***kosa la kimbari*** na ***uhalifu dhidi ya ubinadamu***. Kifungu cha 19(1), (2) na (3) vya ***Sheria ya Mitandao (Cyber Crimes Act, No.14 of 2015),*** sheria inakataza machapisho, uhamasishaji au usambazaji wa vitendo vinavyoweza kusababisha makosa ya kimbari au uhalifu dhidi ya ubinadamu. Kama nikinukuu imeandikwa: -

Kifungu cha 19.-

(1) Mtu hatachapisha au kusababisha kuchapishwa kinyume na sheria vitu vinavyochochea, kanusha, punguza au halalisha matendo yanasababisha **mauaji ya kimbari** na **uhalifu dhidi ya ubinadamu** kwa kupitia mfumo wa kompyuta.

(2) Mtu atakayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, tafsiri ya "**mauaji ya kimbari**" itakuwa na maana kama ilivyo tafsiriwa katika Mkataba wa Kuzuia na Kuadhibu Uhalifu wa Mauaji ya Kimbari wa mwaka 1948 (**Genocide Convention 1948**).

Hata hivyo, bado hakuna sheria inayogusa moja kwa moja mhalifu aliyetenda makosa hayo kwa kuzingatia viini vile vile vinavyozingatiwa na Mahakama ya ICC. Kulingana na uzito wa kosa la kimbari kwa mfano ambalo ni la kuwafuta/kuwateketeza watu wa kundi fulani, au hata uhalifu dhidi ya ubinadamu, nchi nyingine zimeyaainisha kwenye kanuni za adhabu. Mtuhumiwa aliyetenda makosa ya kimbari au uhalifu dhidi ya ubinadamu kwa Sheria zetu atashughulikiwa kama muuaji (endapo amesababisha kifo) au kwa namna nyingine kulingana na matendo yake, lakini hakuna kosa linalounda viini vya makosa hayo kama yanavyotafsiriwa na jumuiya ya umoja wa mataifa pamoja na sheria za Mahakama za kimataifa.

Hata hivyo kwa mfano, kama katika utendaji wa makosa tajwa yatatokea mauaji, sheria zetu tayari zimeainisha adhabu kubwa inayozidi zile zinazotolewa na Mahakama ya ICC (adhabu ya kifo au maisha), lakini ukiondoa umuhimu wa ainisho la viini vya makosa haya wahalifu wengine wanapata mwanya kwasababu viini vya makosa vinavyotambulisha kosa kwenye Kanuni zetu za adhabu ni tofauti na viini vilivyoko kwenye haya.

Kwasababu sio viini vyote vya makosa hayo vimejikita kwenye "**mauaji**", kuna vitendo vingine ambavyo sio vya mauaji lakini ni viini vya makosa hayo, kuna ulazima wa kuyaainisha upya makosa haya kwenye sheria zetu zaidi ya hivi tulivyokwisha fanya. Kwa maana hiyo, hata "**genocide**" haitakiwi kutafsiriwa kama mauaji ya kimbari kwasababu vipo vitendo vingine vinavyounda kosa

hilo ambavyo sio vya mauaji, kama tutakavyoona huko mbeleni. Ingetosha tu kuliita "**kosa la kimbari**".

Makao makuu ya ICC yapo wapi?

Tangu kuanzishwa kwake hadi leo, makao makuu ya Mahakama ya ICC yapo katika mji wa Hague nchini Uholanzi katika bara la Ulaya, na hapo ndipo kesi zinaendeshwa. Hii ilitokana na mapatano yaliyoingiwa kati ya nchi ya Uholanzi na nchi wanachama wa ICC. Hata hivyo, kama zilivyo Mahakama zingine nyingi duniani kuwa na uwezo kuhamia eneo la tukio, Mahakama ya ICC pia inaweza kuhama na kuendesha kesi zake nje ya mji wa Hague endapo majaji wataona ni muhimu na inafaa kufanya hivyo. **Mfn.** Inaweza kuhamia nchi yeyote, hata Arusha Tanzania n.k.

Ni sawa tu na Mahakama zetu hapa Tanzania zinavyoweza kuhamia eneo la tukio na kuendesha kesi huko na uhitaji uliopelekea ihame ukiisha inarudi mahali pake pa kudumu. Vilevile, katika kila eneo ambalo Mahakama inafanya upelelezi/uchunguzi, ofisi za ICC hufunguliwa kwa ajili ya uratibu wa shughuli zinazoendelea.

Mamlaka ya kimipaka ya ICC.

Kiujumla, mamlaka ya kimipaka ya ICC ni kushitaki watuhumiwa toka dunia nzima, ila sera yake kuu ni inalenga kushitaki wahusika wakuu katika kutenda makosa yanayodondokea kwenye mahakama yake. Zifuatazo ni namna kadhaa kimamlaka chini ya Sheria ya ICC: -

(i) Kiujumla, kama maombi yamepelekwa ICC na nchi wanachama mtuhumiwa akiwa ni raia wao au raia wa nchi nyingine aliyetendea kosa kwenye nchi mwanachama, mamlaka ya ICC ni kushughulikia watuhumiwa wa nchi mwanachama tu au waliomuathiri mwanachama.

(ii) Kama maombi ya kuanzisha mchakato yatakuwa yamepelekwa na ***Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa,*** ICC inayo Mamlaka kushitaki wahalifu toka nchi zote hata zile zisizo mwanachama, na hii ni kwa mujibu wa ***sura ya VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter).***[1]

(iii) Kwa kosa la ***uchokozi kwa nchi***, labda kama maombi yamepelekwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ICC inayo mamlaka kushitaki wahalifu toka nchi wanachama tu ambazo pia zimekubali kwa kutia saini kosa hilo lililoanza kufanya kazi tarehe ***17 Juli, 2018***. Wakati wa kuthibitisha kosa la uchokozi kwa nchi, July 2018, nchi wanachama zilipewa uhuru kukubaliana nalo au kulikataa, na hata kwa wale waliosaini kulikubali walipewa uhuru kujiondoa hapo baadaye kwenye kosa hilo tu kama wakitaka, pamoja na kwamba nchi mwanachama hata

[1]Angalia Ibara ya 13 (b) ya Sheria ya ICC.

akiamua kutokukubaliana nalo ataendelea kuwa mwanachama wa ICC aliyekubali makosa mengine nje ya hili.

Na endapo nchi sio mwanachama, au mwanachama ambaye hajasaini kukubaliana nalo, au amesaini na baadaye kujiondoa, ICC haina mamlaka kushughulikia raia wahalifu toka nchini kwake au raia wa nchi nyingine yeyote aliyetendea kosa kwenye nchi hizo. [2]

(iv) Kinyadhifa au vyeo, ICC inashughulikia watuhumiwa wote sawasawa bila kujali nyadhifa alimradi wawe ni wahusika wakuu. Mfano wake ni pale Waandishi wa habari wa **Kenya** waliposhitakiwa sawasawa tu na Rais pamoja na Makamu wa Rais nchini Kenya kutokana na machafuko baada ya uchaguzi mwaka **2007/2008**.

(v) Jambo lingine ni kwamba, ibara ya 16 ya sheria ya ICC inatoa nafasi kwa ***Balaza la Usalama la Umoja wa Mataifa*** kupeleka ombi la kusitisha upelelezi au mashitaka yanayoendelea na ICC, na maombi hayo yafanyikapo, ICC itasitisha upelelezi au mashitaka kwa muda wa miezi 12, na miezi 12 ikiisha Baraza linaweza kupeleka maombi upya; bila kufanya hivyo ICC inaweza kuendelea na upelelezi au mashitaka husika kama ikihitaji kufanya hivyo. Kupeleka maombi hayo yaliyokubalika katika kikao cha Baraza itahitaji uthibitisho wa kura za wajumbe 15 ikijumuisha kura za kukubali na kukataa.[3]

Maombi ya namna hii kwa mujibu wa Sura ya VII ya ***Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter***) na kifungu tajwa hapo juu viliwekwa kwa makusudi ya kuingilia masuala ya aina hii, na mengine mengi ili kuliwezesha *Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa* kulinda au kurudisha amani na usalama kwenye nchi mbalimbali kama itaona kuna vitisho vya amani, uvunjifu wa amani au vitendo vya uchokozi wa nchi.

Na ibara ya 16 ya Sheria ya ICC imetumika kusimamisha upelelezi au mashitaka ya ICC kama itaonekana kuendelea navyo kutachochea zaidi machafuko au matatizo yanayoendelea katika nchi fulani na pengine kusitisha kwa namna hiyo kunaweza kurejesha hali ya usalama. Miezi 12 kimewekwa kama kipindi cha matazamio na tathmini kwa Baraza kuona kama ni muhimu kusitisha au la, kama kikomo cha uhai wa ombi hilo, ikiisha hiyo kama uhitaji utakuwepo Baraza litaongeza miezi mingine 12 na kama litaona hakuna umuhimu litaacha ICC iamue kuendelea na upelelezi/mashitaka ikitaka.

Wanachama wa ICC.

Pamoja na kuwa na nchi nyingi duniani takribani mia moja tisini na tano (195), hadi kufikia *tarehe 17 Machi, 2019* ni nchi 122 tu ndizo wanachama wa ICC, kati ya hizo 33 zinatoka Bara la Afrika, 18 toka Asia Pasifiki, 18 toka Ulaya Mashariki, 28 toka Latin Amerika na Visiwa vya Carebeans na 25 toka

[2]Hii ni kwa mujibu wa **ibara ya 15(4) na (5)** ***bis***

[3]Angalia ibara ya 27 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter).

Ulaya Magharibi na Amerika ya Kaskazini. Zipo nchi nyingine ambazo ziliweka saini lakini mabunge yao hayajapitisha kukubali uanachama na nyingine kama vile Marekani, Israel, Urusi, Sudan n.k si mwanachama kabisa pamoja na kwamba kati ya hizo zipo zilizotia saini makubaliano ya kutoa ushirikiano kwa Mahakama pale itakapohitaji toka kwao.

Utofauti wa ICC na Mahakama nyingine za Kimataifa.

Kabla ya kuundwa kwa ICC, tayari zilishakuwepo Mahakama kadhaa za Kimataifa ambazo ni za muda (ad hoc), tukianzia zile za kivita za Tokyo Japan na Nuremberg Ujerumani mwaka 1945 - 1948 zilizoshughulikia Makosa ya kivita vya pili vya dunia. Mahakama nyingine za muda za hivi karibuni ni

(i) Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Rwanda (ICTR)
(ii) Mahakama ya Kimataifa ya Yugoslavia ya zamani (ICTY),

Zipo mahakama nyingine ambazo pamoja na kwamba zinashughulikiwa kimataifa nap engine kuundwa kwa ushirikiano au msaada wa Umoja wa Mataifa, zingine huchanganya na sheria za nchi zao hivyo wengine kuziita Mahakama za mchanganyiko (hybrid/mixed), mfano: -

(i) **Mahakama maalumu za Lebanon** iliyoundwa kwa makubaliano na Umoja wa Mataifa kushughulikia makosa yaliyotendeka wakati wa mashambulio ya tarehe **14, Februari 2005** yaliyoua watu ishirini na mbili (22) ikijumuisha Waziri Mkuu wa Lebanon Marehemu **Rafik Hariri** na kujeruhi kadhaa. Hii inatumia kanuni za adhabu za Lebanon pamoja na kwamba inashughulikiwa kimataifa. Kituo cha Mahakama hii ni Leidschendam Uholanzi na Ofisi ya ndogo ya Beirut Lebanon.

(ii) **Mahakama maalumu ya Sierra Leon** iliyoundwa kushughulikia makosa yaliyotendeka wakati wa vita za wenyewe kwa wenyewe 1991 – 2002. Hii pia iliundwa kwa ushirikiano na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na inatumia Sheria za kimataifa pamoja na sheria za Siera Leone. Ofisi zake zipo Freetown Sierra Leone, Hague Uholanzi na New York Marekani.

(iii) Kitengo kisicho cha kawaida katika Mahakama za Kambodia (Extraordinary Chambers in the Courts of Cambodia) kilichoundwa baada ya nchi ya Cambodia kuomba usaidizi wa Umoja wa Mataifa kuunda Mahakama kushughulikia makosa yaliyotendeka wakati wa utawala wa **Khmer Rouge** kati ya **1975 -1979**. Pia wafanyakazi wake ni wale wa nchini Kambodia na wengine toka nchi nyingine za kimataifa.

Utofauti wa ICC na Mahakama nyingine za kimataifa ni kwamba, kimipaka, ICC inashughulikia watuhumiwa toka dunia nzima kama watadondokea kwenye masharti ya sheria yake, na pia haina kikomo cha muda alimradi kosa limefanyika baada ya Julai 1, 2002 mkataba wa Roma ulipoanza kufanya kazi. kwa upande wa Mahakama za Kimataifa hizo nyingine ni kwamba, pamoja na kwamba ni za kimataifa lakini sio za kudumu kwani

zikikamilisha mashitaka husika zaweza kufungwa. ICC haitarajiwi kufungwa, ni ya kudumu.

Pia Mahakama nyingine za kimataifa zinashughulikia matukio yaliyotendeka kipindi fulani tu kilichoainishwa, na eneo fulani tu kama lilivyoainishwa kwenye Sheria zao, hazina mamlaka ya kimahakama juu ya ulimwengu wote na muda wote kama ilivyo ICC. ICC iliundwa ili kuondoa dhana ya Mahakama za muda mfupi na zinazofungwa kushughulikia wakosaji wa tukio la eneo fulani tu lilizotendeka kwa kipindi fulani tu, ili kuwe na Mahakama moja tu ya kudumu na itakayoshughulikia dunia nzima.

Mahakama ya Kimataifa ya jinai ya Rwanda (**ICTR**) Arusha Tanzania kwa mfano, kwa miaka kadhaa iliendesha kesi zinazohusiana na makosa ya kimbari na uhalifu dhidi ya ubinadamu yaliyotendeka Rwanda au nje ya mipaka yake kati ya ***Januari 1, 1994*** hadi ***Disemba 31, 1994***; muda kabla na baada ya hapo haina mamlaka. Pia, kijiografia inashughulikia wakosaji waliofanya uhalifu katika kipindi hicho tajwa ndani ya mipaka ya nchi ya Rwanda au raia wa Rwanda waliofanya makosa hayo kwa kipindi hicho katika nchi jirani na Rwanda. Hata hivyo inatarajia kufungwa muda wowote kwani si ya kudumu.

Kwa Ulaya, ipo Mahakama ya Kimataifa ya Yugoslavia ya zamani (**ICTY**) iliyopo Hague Uholanzi ambayo imekuwa ikishughulikia wahalifu wa makosa ya jinai ya kimataifa yaliyotendeka kuanzia January 1, 1991 na kuendelea katika nchi zilizokuwa zinaunda Umoja wa Yugoslavia ya zamani. Mamlaka ya kijiografia kwa Mahakama na muda vimeainishwa kwenye sheria zake.

Utofauti wa ICC na Mahakama ya ICJ.

Pamoja na kwamba ICC na ICJ zote makao yao makuu ni mji wa Hague Uholanzi, ICJ (**International Criminal Justice -Mahakama ya Kimataifa ya Haki**) ambayo wakati mwingine huitwa Mahakama ya dunia ni Mahakama ambayo ni kiungo cha Umoja wa Mataifa kinachoshughulikia migogoro kati ya nchi na nchi, haishughulikii mashitaka dhidi ya watu binafsi kama ilivyo ICC, wakati upande mwingine ICC (**Mahakama ya kimataifa ya makosa ya jinai**) haishughulikii mashitaka/migogoro kati ya nchi na nchi bali inashughulikia watu binafsi (individuals, not states). Kwa maana hiyo mtu aliyefanya mauaji ya kimbari hawezi kushitakiwa ICJ bali ICC; vilevile mgogoro wa mipaka kati ya nchi na nchi hauwezi kupelekwa ICC, utapelekwa ICJ.

Vilevile, wanachama wote wa Umoja wa Mataifa (automatically) ni wanachama wa ICJ ikiwa na maana kwamba, nchi yeyote iliyotia saini mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter) moja kwa moja anakuwa mwanachama wa ICJ [4]. Hata hivyo, nchi ambayo siyo mwanachama wa UN inaweza kuwa mwanachama wa Sheria ya Mahakama hii au kutumia Mahakama kama

[4]Angalia ibara ya 35(1) ya Sheria ya ICJ, inayosema Mahakama itawasikiliza wanachama wake tu, na ibara ya 93(1) ya Mkataba ya Umoja wa Maitaifa (UN Charter) inayosema wanachama wote wa umoja wa mataifa watakuwa wanachama wa Sheria ya ICJ (Statute of the ICJ).

itakubaliana na masharti yaliyowekwa na UN na inakubaliana kuchangia garama za Mahakama hii.

Tofauti nyingine kubwa ni kwamba ili suala lishughulikiwe na ICJ, nchi zilizoko kwenye mgogoro lazima ziridhie kwamba mgogoro wao utatuliwe na ICJ, kama nchi moja itataka na nyingine isitake basi ICJ haina mamlaka kushughulikia mgogoro huo. Kwa upande wa ICC, hii ni Mahakama shurutishi, mtuhumiwa anashurutishwa kupelekwa kule.

Mahusiano kati ya ICC na Umoja wa Mataifa (the UN)

Uhusiano kati ya Umoja wa Mataifa na ICC, kila mmoja anajitegemea na hakuna aliye juu ya mwenzake, na itokeapo maingiliano yeyote ya kiutendaji kati yao ni kwa njia ya makubaliano ya kiushirikiano yaliyoingiwa kati yao kama vyombo viwili huru kila kimoja kikimheshimu mwenzake; hii ni kwa mujibu wa ibara ya 2 ya Sheria ya ICC. Nakala ya mwisho (final draft) ya makubaliano kati ya mihimili hii miwili iliandaliwa tarehe **07/09/2004** na kuruhusiwa katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa tarehe **13/09/2004** Azimio 58/318 (**Resolution 58/318**).; mwisho kabisa viongozi wawili toka pande zote walitia saini, kwa upande wa ICC waliwakilishwa na Rais wa ICC ***Judge Philippe Kirsch*** na kwa upande wa Umoja wa Mataifa waliwakilishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakati huo marehemu ***Kofi Annan***. Kwa kifupi, makubaliano ya uhusiano kati ya mihimili hii miwili ipo katika Nyanja zifuatazo: -

(1) Kuonyesha njia rahisi katika kubadilishana wawakilishi, kubadilishana taarifa na nyaraka, ushirikiano wa kiutawala, matumizi ya kumbi za mikutano matumizi ya vitambulisho/vibali maalumu vya kusafiria kwa watumishi maalumu wa Umoja wa Mataifa ambavyo vinaweza kuwajumuisha na baadhi ya watumishi wa ICC.

(2) Ushirikiano katika kushughulikia makosa ya jinai ya kimataifa, hii ikijumuisha kutoa taarifa za matukio ya kihalifu na jinsi Baraza la Uslaama la Umoja wa Mataifa linavyoweza kupeleka maombi ya kupeleleza au kushitaki chini ya ibara ya 13(b) ya Sheria ya ICC

(3) Pia maombi ya kusitisha upelelezi au mashitaka yanayofanywa na ICC kwa mujibu wa ***ibara ya 16 ya Sheria ya ICC*** na ***ibara ya 27 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa***.

(4) Makubaliano haya pia yanaainisha ushirikiako kati ya Mwendesha Mashitaka Mkuu wa ICC na Umoja wa Mataifa, pamoja na suala la kinga, ulinzi na utunzaji siri.

Je? ICC ni mbadala wa Mahakama zetu za ndani?

Jibu ni **"HAPANA",** nia ya awali kuunda Mahakama hii na sera yake hadi sasa sio kuzibadili Mahakama zetu za ndani ya nchi, pamja na kwambakama nchi husika haina nia kushughulikia wahalifu, haina uwezo kushughulikia au

inashughulikia kama gelesha ya kumkinga mtuhumiwa asipelekwe ICC n.k, Mahakama hii ionaonekana kama mbadala kwasababu itaingilia kati na kushughulikia mtuhumiwa husika, na kufanya lile jambo nchi husika haijafanya.

Kwa mujibu wa Sheria ya ICC, wajibu wa kwanza kabisa kushughulikia mtuhumiwa aliyetenda makosa yanayodondokea kwenye mahakama yake upo mikononi mwa nchi husika, ICC haisimami kama mbadala wa moja kwa moja wa Mahakama zetu za ndani. Endapo nchi husika itachukua hatua za upelelezi au mashitaka ambazo zina nia ya dhati na sio gelesha kumkinga mtuhumiwa na ICC, Mahakama hii haina mamlaka kabisa kushitaki mtuhumiwa husika.

Tukisoma ***Aya ya 10*** ya dibaji/ Preamble na ***Ibara ya 1*** na ya ***17*** za Sheria ya ICC vinaeleza kwamba, kipaumbele cha kwanza cha kushughulikiwa watuhumiwa kipo mikononi mwa nchi husika, na ikishindikana ndipo ICC itakuwa na mamlaka kuingia na kushughulikia tuhuma husika. ICC haijaundwa kuwa mbadala wa moja kwa moja wa Mahakama zetu labda kama nchi husika haijatimiza wajibu wake wa kisheria.

Kwa kawaida kisheria inasemekana haki inatakiwa sio tu kutendeka bali ionekane imetendeka. Ikiwa nafasi hii itatumiwa na nchi mwanachama kumshitaki mtuhumiwa kwa gelesha tu kwa nia ya kumlinda asipelekwe ICC (ili Mahakama ya ICC ione ameshashughulikiwa na nchi husika hivyo haina mamlaka kuingilia kati), Mahakama hii imepewa mamlaka kumshitaki tena huyo mtuhumiwa.

Ni wajibu kwa nchi wanachama, na hata zile zisizo mwanachama, kutumia mifumo yao ya utoaji haki ndani ya nchi zao kushughulikia watuhumiwa kwa mujibu wa sheria zao pasipokuwa na gelesha, na Mahakama hii itakuwa imefungwa mikono kuwakamata na kuwashitaki tena.

Mazingira yafuatayo yanaifanya ICC isiwe na mamlaka.!

Ibara ya 17 ya Sheria ya Mahakama ya ICC inaeleza kwamba, Mahakama ya ICC haitakuwa na mamlaka kupokea na kuendesha upelelezi au mashitaka ya kesi katika mazingira yafuatayo; -

(1) ***Ukiwepo ushahidi kwamba kesi ya mtuhumiwa husika inapelelezwa katika nchi husika au mashitaka yamefunguliwa/yanaendelea katika mahakama zenye mamlaka katika nchi husika.*** Hata hivyo ICC inaweza kuingilia kati kama pamoja na kufanya hivyo nchi husika **haina nia thabiti** au **uwezo** kuendesha upelelezi na mashitaka.

(2) ***Kama kesi imepelelezwa na nchi husika yenye mamlaka na kesi hiyo na nchi hiyo imeamua kutokumshitakimtuhumiwa labda kwasababu hakuna ushahidi wa kutosha.*** ICC hailazimishi mtu kufunguliwa mashitaka hata kama hakuna ushahidi wa kutosha, ndio maana haya yenyewe kabla usikilizwaji kamili kuanza lazima kitengo cha awali

kiendeshe kesi ya uthibitishwaji wa kosa, kama mashitaka yana mashiko au la.

(nia ya kumshitaki inaweza ikawepo na inaonekana kwa macho ya kisheria, lakini ushahidi ukawa hautoshi; lakini kama kesi imepelelezwa na ushahidi upo lakini nchi husika haina nia ya kumshitaki au haina uwezo wa kumshitaki, ICC itaingilia kati; haimaanishi kuwa ICC inalazimisha mtu afunguliwe mashitaka hata kama ushahidi hakuna).

(3) ***Kama Mtuhumiwa husika ameshashitakiwa na Mahakama za nchi kutokana na Makosa yaleyale;*** ISIPOKUWA kama uendeshaji wa kesi hiyo ulifanywa sio kwa nia ya kutafuta haki bali kwa nia ya kumkinga asifikishwe ICC, au kama mashitaka hayakuendeshwa kwa uhuru, bila upendeleo na kwa misingi ya haki zinazokubalika Kimataifa na yaliendeshwa kwa nia na mazingira ambayo si ya kufanya haki itendeke.

(4) ***Kama kesi haina viini vyenye uzito kuendeshwa na Mahakama ya ICC***. Hapa maana yake ni kwamba, ICC haishughulikii kila kosa; yenyewe inashughulikia makosa yale tu ambayo jumuiya ya kimataifa imeyaona ni mazito kupindukia yanayotishia usalama, ustawi na amani ya watu duniani yaani ***makosa ya kimbari, uhalifu dhidi ya ubinadamu, makosa ya kivita*** *na* ***kosa la uchokozi kwa nchi***. Nje ya hapo, hata kama tukio litakuwa limesababisha mauaji ya raia, kama hakuna viini vinavyodondokea kwenye makosa hayo, Mahakama hii haina mamlaka kushughulikia.

Nini maana ya Nchi Kutokuwa na Nia ya kushitaki?

Ibara ya 17 (2)(a)-(c) ya Sheria ya ICC imefafanua mazingira yanayoweza kuifanya ICC kuitambua nchi husika kama haina nia ya kweli kumshughulikia mkosaji na hivyo kuifanya ICC iingilie kati: -

(a) Mazingira yanaonyesha kuwa mashitaka yalishafanyika au yanaendelea kufanyika, lakini yalifanyika tu kwa nia ya kumkinga mtuhumiwa asishitakiwe chini ya Makosa yanayodondokea Mahakama ya ICC.

(b) Kuna ucheleweshaji usio wa msingi kumshitaki mtuhumiwa au katika uendeshaji wa kesi, wenye viashiria kwamba nchi husika haina nia ya dhati kufanya haki itendeke dhidi ya mtuhumiwa.

Mfano mzuri hapa ni nchi ya Kenya baada ya fujo za uchaguzi 2007/2008; zaidi ya mwaka mmoja ulipita bila kushughulikia watuhumiwa katika Mahakama za Kenya pamoja na viongozi wa Kimataifa na jumuiya ya Kimataifa kuishawishi sana Kenya kulishughulikia suala lao kwa kutumia mfumo wa kimahakama wa Kenya. Baada ya kusuasua sana na kuonyesha kana kwamba nia ya dhati kutumia Mahakama za Kenya haipo, **tarehe 26/11/2009** Mwendesha Mashitaka kama ulivyo utaratibu,

aliomba ruhusa kuanzisha upelelezi katika matukio yaliyojiri baada ya uchaguzi wa Kenya wa **mwaka 2007/2008**.

Hii ilikuwa ni kwasababu ya ucheleweshwaji usio na msingi kushughulikia watuhumiwa. Laiti kama nia ya kutumia Mahakama za palepale Kenya ingedhihirishwa kwa vitendo na kwa wakati, viongozi wa Kenya pamoja na waandishi wa habari wasingepata shuruba za ICC kama tulivyoshuhudia.

(c) Mashitaka hayakuendeshwa au hayaendeshwi kwa uhuru au bila upendeleo na mazingira yalionyesha/yanaonyesha kuwa, mashitaka dhidi ya mtuhumiwa hayakuwa kwa nia ya kuhakikisha haki inatendeka dhidi ya mtuhumiwa. (hapa uhuru wa Mahakama na vyombo vya kiupelelezi chaweza kuwa kipimo).

Nini maana ya Nchi kutokuwa na Uwezo?

Ibara ya 17(3) ya Sheria ya ICC inaeleza kwamba, tathmini kama nchi husika imekosa uwezo kushughulikia mtuhumiwa kwa njia ya vyombo vya kisheria, yaweza kupimwa kwa kuangalia ujumla au kiwango fulani cha kusambaratika au kutokuwepo kwa mfumo wa kimahakama, kutokuwa na uwezo kumtafuta na kumkamata mtuhumiwa au kukusanya ushahidi muhimu na mashahidi au na pengine kutokuwa na uwezo kuendesha mashitaka. Mfano mzuri wa kutokuwa na uwezo ni kwa nchi ambazo zimesambaratika na mifumo ya utoaji haki imesambaratika kama ilivyokuwa Somalia kipindi cha nyuma na nchi zenye mfano huo. Mazingira kama hayo ICC itaingilia kati.

Watu toka nchi zipi wanaweza kushitakiwa na ICC?

Kwa kuzingatia makosa yaliyotendeka kuanzia tarehe **01/07/2002** na kuendelea (kwasababu kwa misingi ya sheria mtu hatakiwi kushitakiwa kwa kosa ambalo sheria inayotumika haikuwa imetungwa wakati alipotenda kosa hilo (non-retroactive principle *ibara ya 24 ya Sheria ya ICC*), aina za watu wafuatao wanaweza kushitakiwa katika Mahakama ya ICC: -

(i) **Watuhumiwa raia wa nchi mwanachama**, au wale wasiotoka nchi mwanachama lakini wametendea kosa kwenye nchi mwanachama. Hata hivyo, sharti hili kubwa linazingatiwa pale tu ambapo ombi la kushughulikia mtuhumiwa limepelekwa ICC na nchi mwanachama au mwendesha mashitaka mwenyewe kwa uamuzi wa binafsi ameanzisha mchakato wa kiupelelezi. Angalia ibara ya 13(a), (b) a (c) ya Sheria ya ICC.

(ii) **Raia yeyote wa nchi yeyote hata zile zisizo mwanachama wala makosa kutendeka katika nchi mwanachama**, kama ombi la mchakato wa kushughulikia tuhuma litakuwa limepelekwa ICC kwa Azimio la Kikao cha **Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa** (UN Security Council Resolution) chini ya Sura ya VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa (the UN Charter). Tatizo linakuja pale ambapo mtuhumiwa anayetoka nchi isiyo mwanachama (mfano USA, CHINA, URUSI, SUDAN n.k) ametenda kosa hilo kwenye nchi

isiyo mwanachama na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa halijaazimia kupeleka jambo hilo ICC; Mtuhumiwa huyo anaweza kupona mashitaka na ICC haitakuwa na nguvu kumshughulikia.

Mfano ni Rais wa zamani wa Sudan, **Rais Al Bashir** alituhumiwa kutenda makosa nchini kwake Sudani, na Sudani sio mwanachama wa Mahakama ya ICC; hakuna nchi yeyote iliyokuwa na uwezo kisheria kulipeleka suala hilo ICC, wala Mwendesha mashitaka kisheria hakuruhusiwa kuanzisha mchakato yeye mwenyewe, hadi pale Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipotoa Azimio la kupeleka maombi ICC ndipo mchakato wa kutoa hati ya kumkamata ulianza. Kama Balaza la Usalama lisingefanya hivyo hakuna chombo kingine kisheria ambacho kingeisukuma ICC kuanzisha mchakato dhidi ya Rais Omar Al Bashir.

(iii) Kwa kosa la ***uchokozi kwa nchi***, labda kama ombi limepelekwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ICC inayo mamlaka kushitaki wahalifu toka nchi wanachama tu ambazo pia zimekubaliana kwa kutia saini kosa hilo lililoanza kufanya kazi tarehe 17 Juli, 2018, au hata kama mtuhumiwa ametendea kosa kwenye nchi mwanachama, atashughulikiwa kama nchi iliyotendewa imetia saini kulikubali kosa hili. Wakati wa kuthibitisha kosa hili July 2018, nchi wanachama zilipewa uhuru kusaini kukubaliana nalo au kulikataa kwa kutokusaini, na hata kwa wale waliosaini walipewa uhuru kujiondoa hapo baadaye kwenye kosa hilo tu kama wakitaka, pamoja na kwamba nchi mwanachama hata akiamua kutokukubaliana nalo ataendelea kuwa mwanachama wa ICC kwa kuwa chini ya makosa mengine nje ya hili.

(iv) Katika kosa hili la uchokozi kwa nchi, endapo nchi sio mwanachama, au mwanachama ambaye hajasaini kukubaliana nalo, au amesaini na baadaye kujiondoa, ICC haina mamlaka kushughulikia raia wahalifu toka nchini kwake au raia wa nchi nyingine yeyote aliyetendea kosa kwenye nchi hizo labda kama ombi limepelekwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Matiafa. [5]

(v) Kwa jicho la aina ipi ya watuhumiwa kivyeo, ICC haina mipaka ya nyadhifa/vyeo, inashughulikia watuhumiwa wote sawasawa bila kujali nyadhifa au vyeo isipokuwa inalenga wahusika wakuu peke yake.

(vi) Jambo lingine ni kwamba, ibara ya 16 ya sheria ya ICC inatoa nafasi kwa ***Balaza la Usalama la Umoja wa Mataifa*** kupeleka ombi la kusitisha upelelezi au mashitaka yanayoendelea na ICC, na maombi hayo yafanyikapo, ICC itasitisha upelelezi au mashitaka kwa muda wa miezi 12. Hata hivyo, miezi 12 ikiisha Baraza linaweza kupeleka maombi upya, bila kufanya hivyo ICC inaweza kuendelea na upelelezi au mashitaka husika kama ikihitaji kufanya hivyo. Kupeleka maombi hayo yaliyokubalika katika kikao cha Baraza itahitaji uthibitisho wa kura za wajumbe 15 ikijumuisha kura za kukubali na kukataa.[6]

---

[5] Hii ni kwa mujibu wa **ibara ya 15(4) na (5)** ***bis***

[6] Angalia ibara ya 27 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter).

Nani anaweza kukwepa kupelekwa ICC?

Kwa maelezo tuliyokwishaona hapo juu, ni vigumu wahusika wakuu wa jinai kuikwepa ICC moja kwa moja, awe ametoka nchi mwanachama au la; labda tu anaweza kukwepa kukamatwa baada ya amri ya kumkamata kutolewa, kwa kutotembelea nchi mwanachama wa ICC zenye wajibu wa kutoa ushirikiano kwa ICC. Pamoja na kwamba ICC imeonekana kukosa meno kwa nchi wanachama wanaoshindwa kutoa ushirikiano, mfano; kukamata wakosaji wanaotembelea nchi zao, lakini iko wazi watuhumiwa wamepata usumbufu na kukosa uhuru kutembelea nchi mbalimbali duniani kwa woga wa kukamatwa, jambo ambalo tukubali kuwa ni adhabu kwao pia.

Woga huu umeendelezwa pia na kutokuwa na imani na tawala zitakazokuja mbeleni kama wataamua kushirikiana na ICC kwa kumkabidhi mtuhumiwa ambaye pengine hawakukubaliana naye alipokuwa kwenye nyadhifa fulani. Kiujumla, hata pale ambapo si nchi mwanachama wala Mwendesha Mashitaka wa ICC watakuwa wameanzisha tuhuma, bado Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linaweza kuazimia kuiomba ICC kupeleleza tukio lenye viashiria vya makosa haya. Hivyo, nchi iwe mwanachama au la, raia wake kwa namna moja ama nyingine hatakwepa moja kwa moja kushitakiwa ICC kama akiwa kwenye mianya yote ya kushitakika katika sheria ya ICC.

Namna mashitaka yanavyoanzishwa/fikishwa ICC

Namna ya kupeleka mashitaka ICC sio sawa na namna mashitaka yanavyopekekwa kwenye vyombo vya Sheria vya Tanzania. Hapa Tanzania mlalamikaji atapeleka mashitaka Polisi ambapo jalada litafunguliwa na upelelezi na kukamatwa kwa mtuhumiwa kutafuata, na mwisho jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashitaka (Ofisi ya DPP) ili kutathimini kama ipo kesi ya kujibu hivyo mashitaka yafunguliwe Mahakamani au hakuna ushahidi kesi ifungwe au upelelezi zaidi ufanyike kipengele fulani.

Kwa upande wa ICC, kuna namna tatu (3) tu kuanzisha mashitaka chini ya ***ibara ya 13(a) (b) na (c)***; -

1) Ombi kupelekwa Ofisi ya Mwendesha Mashitaka na nchi mwanachama wa mkataba wa Roma (mwanachama wa ICC).

2) Mwendesha mashitaka mwenyewe kuanzisha mchakato bila kusukumwa na yeyote.

3) Balaza la Usalama la Umoja wa Mataifa kupeleka suala hilo Ofisi ya Mwendesha Mashitaka baada ya Azimio chini ya Sura ya VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Watu binafsi, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali n.k, wanaweza kupeleka suala ICC kama taarifa tu kuonyesha uwepo wa makosa fulani kama yametendeka ili Mwendesha Mashitaka aanzishe au nchi wanachama au Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wapeleke maombi maalumu.

Vilevile ***Ibara ya 15 (6) na 53(2) vya sheria ya ICC***, vinaeleza kwamba, kama baada ya taarifa au maombi kupelekwa Mwendesha Mashitaka amefikia hitimisho kwamba hakuna umuhimu kuendelea na mchakato, atawapatia taarifa/mrejesho wale walioleta taarifa au maombi kuhusu tukio husika.

Mwendesha mashitaka kuanzisha mchakato yeye mwenyewe?

Mwendesha Mashitaka wa ICC huchaguliwa na nchi wanachama**.** [7]Ibara ya **13(c), 15 na 53(1) – (4) vya Sheria ya ICC** vinatoa nafasi kwa Mwendesha Mashitaka yeye mwenyewe bila kuletewa maombi na yeyote, kuanzisha mchakato wa upelelezi hadi mashitaka akiwa na taarifa za kuaminika (ziwe taarifa za wazi au za siri) kuwa mojawapo ya Makosa yaliyopo kwenye Sheria ya ICC yametendeka katika nchi fulani. Yanaweza kuwa yametendeka kwenye nchi mwanachama au isiyo mwanachama lakini imekubali mamlaka ya kimahakama ya ICCkwa Makosa yaliyofanyika nchini mwake.

Ibara ya 15 ya Sheria ya ICC inaeleza kwamba,

1. Mwendesha Mashitaka anaweza kuanzisha upelelezi yeye mwenyewe kutokana na taarifa za tuhuma zinazodondokea kwenye makosa chini ya ICC.

2. Mwendesha Mashitaka atatathimini uzito wa taarifa alizozipokea, na anaweza kuomba taarifa za ziada za tukio toka nchi wanachama, organs of the United Nations, mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali au vyanzo vingine vya kuaminika na anaweza kupokea taarifa za kiushahidi za maandishi au za mdomo kwenye kituo cha Mahakama hiyo.

3. Mwendesha Mashitaka akifikia hitimisho kwamba kuna sababu za msingi kuendelea na upelelezi, atapeleka ombi hilo Kitengo cha awali cha usikilizwaji (Pre-Trial Chamber) ombi la kuruhusu upelelezi akiambatanisha ushahidi wowote uliokusanywa naye kabla ya hapo. Mbele ya kitengo hicho cha awali cha usikilizwaji, waathirika wanaweza kufanya uwakilishaji kwa mujibu wa Kanuni za Kiutaratibu na Ushahidi za Mahakama (Rules of Procedure and Evidence).

4. Kitengo cha usikilizwaji wa awali, baada ya upembuzi wa taarifa hizo na vyote vinavyoziunga mkono kama wataona kuna sababu za msingi kuendelea na upelelezi, na kama kesi inadondokea kwenye mamlaka ya Mahakama, itaruhusu upelelezi kuanza kwa kuthibitisha kwamba kuna sababu za msingi za tuhuma. Hata hivyo hii haitaathiri maamuzi mengine ya baadaye ya Mahakama kuhusiana na mamlaka na upokelewaji Mahakamani wa kesi husika.

5. Kama kitengo cha awali kitakataa kuruhusu Mwendesha Mashitaka kuendelea na upelelezi, Mwendesha mashitaka anaweza kuleta maombi

[7]Ibara ya 42(4) ya Sheria ya ICC

mapya hapo mbeleni kama atakuwa amepata hoja au ushahidi mpya kuhusiana na tuhuma zilezile alizokuwa amezileta awali.

6. Kama katika upembuzi wa awali wa taarifa zilizofikishwa kwa Mwendesha Mashitaka, ameona taarifa zilizofikishwa sio za msingi kuanzisha upelelezi, atawataarifu wale walioleta taarifa kwake. Hii haitamzuia Mwendesha Mashitaka kuzingatia taarifa mpya na ushahidi mpya nyingine zitakazoletwa kwake kuhusiana na tukio lilelile.

Mfano: **tarehe 26 Novemba, 2009**, mwendesha mashitaka yeye mwenyewe bila kusukumwa na vyombo vingine, aliiomba mahakama kibali kufungua kesi ya uchunguzi wa matukio yaliyotokea ***Kenya***baada ya **uchaguzi wa 2008**. Pre-trial chamber II walimpatia kibali hicho tarehe 31 Machi 2010. Vilevile, **Tarehe 03 Octoba 2011,** mwendesha mashitaka alipewa kibali na *kitengo cha usikilizwaji wa kabla III* kufungua uchunguzi/upelelezi katika matukio yaliyotokea baada ya uchaguzi wa ***Ivory Coast*** na aliyekuwa Rais wa nchi hiyo alishitakiwa.

Maombi kupelekwa na nchi mwanachama

Ibara ya 14 (1) na (2) inaeleza kwamba: -

1. Nchi mwanachama inaweza kupeleka ombi kwa Mwendesha Mashitaka kuhusu tukio moja ama zaidi yanayodondokea kwenye mamlaka ya ICC yanaonekana yametendeka, akimwomba Mwendesha Mashitaka kupeleleza ili kutathimini kama mtu mmoja au zaidi wanatakiwa kushitakiwa kutokana na kutenda makosa husika.

2. Mapema iwezekanavyo, taarifa hiyo ifafanue mazingira husika yanayoambatana na nyaraka zinazounga mkono ombi, ambazo nchi hiyo inayoleta ombi inazo.

Nchi gani mwanachama ilishapeleka maombi ICC?

Zipo nchi kadhaa mwanachama ambazo nyingi zinatoka Bara la Afrika ambazo zenyewe na kwa hiari yake zilishapeleka maombi kwa Mwendesha Mashitaka ili upelelezi uanzishwe kwa watuhumiwa raia wa nchi zao au wale waliotendea makosa katika nchi wanachama. Zifuatazo ni mifano kadhaa tu.

(1) **Nchi ya Mali ambayo wananchi wake wawili wamepelekwa ICC**. Watuhumiwa hawa walitokana na vita iliyoendeshwa na wanamkambo wa kiislam wa Tuareg kaskazini mwa Mali, Azawad, mapigano yaliyopelekea pia kupinduliwa Rais wa nchi na jeshi kwa kile walichoamini ameshindwa kuwadhibiti waasi hao. Mali ilipeleka maombi ICC tarehe 16 June 2012 na uchunguzi ulianzishwa na ICC tarehe 16 January, 2013. Tarehe 22 Agosti 2016 usikilizwaji wa mtuhumiwa mmoja wapo ***Ahmad Al Faqui AI Mahdi*** mwanachama wa ***Ansar Eddine*** chenye ushirika na ***Al Qaeda*** ulianza, na tarehe 27 Septemba, 2016 *Trial Chamber VIII* ilimkuta *Mr. Mahdi* na hatia

ya kutekeleza mashambulizi kwenye makumbusho ya historia za kidini yaliyokuwa yanatambuliwa kama hifadhi na UNESCO.

Mtu mwingine wa Mali ni ***Al Hassan Ag Abdoul Aziz Ag Mohamed Ag Mahmoud***, ambaye kesi yake bado inaendelea hadi sasa (mwaka huu 2020), anasemekana kutoka katika kundi la ***Ansar Eddine*** pia akiwa na nafasi kama Mkuu wa Polisi katika dola ya Kiislam waliyokuwa wanatarajia kuiunda eneo hilo. Tarehe 31 Machi, 2018 alifunguliwa mashitaka ICC ya ***Uhalifu dhidi ya ubinadamu*** na ya ***kivita*** yaliyojumuisha unyanyasaji wa kingono na kijinsia alioufanya eneo la Timbuktu nchini humo kinyume na ibara ya 8(2)(e)(vii) vya Sheria ya ICC.

(2) **Nchi ya Uganda.** Uganda ambayo pia ni mwanachama wa ICC, kutokana na vita vyake na waasi wa LRA (Lords Resistance Army) chini ya Joseph Kony, mnamo tarehe 16 December, 2003 ilipeleka maombi ICC ili upelelezi na mashitaka yafanyike dhidi ya ***Joseph Kony, Raska Lukwiya, Okot Odhiambo, Dominic Ongwen*** *na* ***Vicent Otti***.

(3) **Nchi ya DR Congo**. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo ambayo pia ni mwanachama ilipeleka maombi ICC tarehe 19 April, 2004 ambapo Mwendesha mashitaka alianzisha uchunguzi tarehe 23 Juni, 2004. Hadi sasa watuhumiwa walioshughulikiwa ICC tokea DR Congo ni *Mathieu Ngudjolo Chui, Germain Katanga, Thomas Lubanga Dyilo, Callixte Mbarushimana, Sylvestre Mudacumura na Bosco Ntaganda.*

(4) **Nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati (Central African Republic).** Mnamo tarehe 22 Disemba, 2004 ilipeleka maombi dhidi ya *Jean Pierre Bemba Gombo* na wenzake. Bwana Bemba raia wa DR Congo aliyefanya mashambulizi kinyume na sheria katika nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati. Bemba alishashitakiwa na ICC. Katika nchi hiyohiyo, yalitokea mapigano ya kidini kati ya Wakristo na Waislam na mwendesha mashitaka yenye mwenyewe alishafungua upelelezi wa makosa ya jinai yaliyotendeka katika machafuko hayo. Hata hivyo, hadi sasa hakuna mtuhumiwa yeyote ambaye amekwishafunguliwa mashitaka kutokana na mapigano hayo ya kidini.

Hii ni mifano ya nchi baadhi tu. Bila kusahau nyingine ambazo ziko kwenye mchakato wa upembuzi, kama *Gabon*. Kwa ulimwengu mzima, nchi za Afrika ndizo zimepeleka zenyewe maombi ICC dhidi ya watu wao kwa wingi kuliko wengine, jambo linalopunguza hata uzito wa dhana kwamba ICC inashughulikia Waafrika tu kwasababu wao wenyewe wamejipeleka na baadaye wanalalamika kwamba wanashughulikiwa. Hata hivyo, kwasababu kipaumbele cha kwanza zimepewa nchi husika labda kama zitapenda kupeleka ICC au zitakuwa zimeshindwa au kutokuwa na nia ndio ICC huingilia kati, wengine wanaweza kusema Afrika haiathiriki chochote na hailengwi pekee, kwasababu wote waliopelekwa huko walizungukwa na tuhuma nzito za kiushahidi. Zaidi ya yote, mtenda mabaya anaposhughulikiwa huwezi kusema

unaonewa kwasababu alipokutendea mabaya ulikuwa unalalamika na ulikimbilia kushitaki ICC wewe mwenyewe.

Je? Balaza la Usalama la Umoja wa Mataifa walishapeleka suala ICC?

Hadi leo Balaza la Usalama la Umoja wa Mataifa chini ya ***Sura ya VII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa*** wameshapeleka maombi ya aina hii dhidi ya Rais wa zamani wa Sudani ***Mh. Al Bashir*** kuhusiana na tuhuma za Mauaji ya Kimbari jimbo la *Darful*, na pia tuhuma za uvunjifu wa sheria za kimataifa katika matukio ya Libya Februari, 2011. Hiyo ni mifano tu kwamba inaweza kufanya hivyo.

Nini hutokea suala likipelekwa ICC kwa ajili ya upelelezi?

Kinachotokea ni kwamba, Mwendesha Mashitaka hufanya tathimini kama ifuatavyo: -

(1) Ataangalia kama ICC inayo mamlaka kushughulikia tuhuma hizo, kwa kuangalia mamlaka ya mipaka iliyoweka katika Sheria ya ICC na uzito wa kosa n.k. Kwa umakini kabisa, taarifa iliyopo itapimwa kuangalia kama kuna sababu za msingi kuendelea na upelelezi ama la. Ni lazima ajihakikishe kwamba moja wapo ya Makosa yanayoshitakika katika Mahakama ya ICC yametendeka, yaani **Makosa ya Kimbari**, **Uhalifu dhidi ya ubinadamu**, **Makosa ya kivita** na kosa la **Uchokozi wa nchi**.[8]

(2) Vilevile, Mwendesha Mashitaka lazima ajihakikishe kama makosa yanayotuhumiwa yametendeka kuanzia tarehe 1 Julai 2002 na kuendelea na si kabla ya hapo**.**

(3) Vilevile, mwendesha mashitaka lazima aangalie, kulingana na **aya ya 10** ya **dibaji**, **ibara ya 1 na 17ya Sheria ya ICC** kama nchi husika inaendesha upelelezi wa uhakika au mashitaka kuhusiana na tukio husika. Kama kitu kama hicho kinaendelea ICC imefungwa mikono, haina mamlaka kuingilia.

(4) Mwisho lazima azieleze nchi zote mwanachama wa ICC na zile zilizokubaliana kushirikiana na Mahakama, nia yake kuanzisha upelelezi.

(5) Atapeleka ombi la kuanzishwa upelekezi kwenye kitengo cha awali cha usikilizwaji (Pre-Trial Chamber) watathimini kama kuna umuhimu watoe ridhaa kuendelea na upelelezi au la**.**

(6) Kama kitengo cha usikilizwaji awali kitaona kuna sababu za msingi kuanzisha upelelezi, na wakatoa ridhaa hiyo, hapo ndipo upelelezi huanzishwa hadi usikilizwaji wa kesi kama atakavyoona inawezekana.

[8]Angalia ibara ya 15(4) na (5) *bis* ya sheria ya ICC

(7) Amri ya kukamata mtuhumiwa ili afike mbele ya Mahakama inaweza kutolewa baada ya maombi ya Mwendehsa Mashitaka kama itaonekana mtuhumiwa ni mkaidi, lakini kama mtuhumiwa anaonyesha kutoa ushirikiano kufika mwenyewe, hutolewa samansi za kumtaka afike yeye mwenyewe kwa hiari yake.

Je? Inawezekana jambo la kupelekwa ICC likapitwa na wakati?

ICC inayo mamlaka kushughulikia Makosa yaliyotendeka kuanzia Sheria yake ilipoanza kufanya kazi *Julai 1, 2002* na kuendelea bila kikomo. Makosa yaliyotendeka kabla ya hapo ICC haina nguvu kisheria kushughulikia. Hivyo, maadamu kosa lilitendeka baada ya tarehe *01 Juli, 2002*, na vigezo vyake vimetimia kuunda Makosa yaliyoko kwenye sheria ya ICC kiuzito na kwa kutimiza masharti ya kimashitaka na kisera, hakuna kikomo cha muda wa kushughulikia jinai husika. Kama mtuhumiwa hajashughulikiwa leo anaweza kushughulikiwa muda wowote miaka yoyote ijayo. ***ibara za 24 na 29***).

Nani anaweza kushitakiwa ICC?

Sera ya ICC ni kushitaki wahusika wakuu zaidi katika kosa (***those who bear the greatest responsibility for the crimes***). Kwa jicho la namna hiyo, mtu yeyote, bila kujali cheo/wadhifa anaweza kushitakiwa ICC alimradi ni mhusika mkuu. Watuhumiwa wanaweza kuwa ni wengi sana na ICC haiwezi kushughulikia kila mtu, ingezidiwa kama ndio hivyo.

Mfano, tuchukulie labda nchini DR Congo ambako kuna vita nyingi zinaendelea; kikundi cha uasi chenye wafuasi 3,000 kimefanya mauaji ya halaiki au kimbari, ICC haiwezi kushitaki wote 3,000, Ofisi ya Mwendesha Mashitaka inatakiwa kuchagua wahusika wakuu tu waliowajibika zaidi hadi kosa kutendeka. Wanaweza kuwa wale walioongoza wengine kutenda kosa, wale waliohamasisha kwa njia mbalimbali, viongozi wa wengine waliozembea kuzuia, kusimamisha au kuwajibisha walio chini yao baada ya kosa kutendeka.

Hata hivyo, ibara ya 26 ya sheria yaICC inaeleza kwamba ICC haishughulikii mashitaka dhidi ya yeyote aliye chini ya ***miaka 18 wakati alipotenda kosa (watoto).*** Pia, msamaha wowote hata kama ni wa rais wa nchi, hauwezi kumfanya mtu asishitakiwe na ICC, labda kama mchakato wa kisheria ulifanywa kwa uwazi na bila upendeleo.

Hatua kwa hatua mwenendo kuanzia kosa kutendeka

Taarifa ya jinai: - Baada ya jinai kutendeka na maombi ya mashitaka au taarifa kumfikia Mwendesha Mashitaka wa ICC na nchi mwanachama, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa au Mwendesha Mashitaka kuamua kuanza yeye mwenyewe yafuatayo yatafanyika.

(1) Atakusanya taarifa za awali za kumwezesha kujenga hoja za msingi mbele ya Kitengo cha awali cha usikilizwaji kuruhusu upelelezi kuanzishwa.

(2) Mwendesha Mashitaka atatathimini kuona kama lina viini vinavyodondokea makosa manne (4) yanayoendesha na ICC, na ataandaa maombi kupeleka mbele ya kitengo cha usikilizwaji wa awali.

(3) Kama nchi husika ilishaanza upelele au/na mashitaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa husika ambayo sio gelesha, anaweza asiendelee na mchakato.

(4) Endapo nchi husika itakuwa haijafanya lolote kwa kitambo cha kutosha, Mwendesha mashitaka atatathimini pamoja na hayo mengine kama kuanzisha upelelezi hadi mashitaka yapo maslahi ya haki na ya waathirika kuendelea na kesi.

(5) Kama mwendesha mashitaka katika upelelezi wake ataona ushahidi haupo, nchi husika imeshaanzisha upelelezi na mashitaka (ambayo sio gelesha), nchi husika imepeleleza na kuona hakuna kosa la jinai lililotendeka (na ICC kujiridhisha hivyo katika upelelezi wake), ataishia hapo, hataendelea na hatua zinazofuata pamoja na kwamba atataarifu vyombo vilivyoleta taarifa kwake kwanini hajaendelea.

(6) Kama ushahidi unaonyesha viini vya makosa vipo na nchi husika haijamshughulikia mtuhumiwa kwenye vyombo vyake vya sheria kwa kitambo cha kutosha, au imemshughulikia lakini kwa gelesha tu kumlinda asishughulikiwe na ICC, mwendesha Mashitaka atapeleka ombi kwenye kitengo cha Majaji wa usikilizwaji wa awali (Pre-trial Chamber) akiomba Majaji kuthibitisha kwamba zipo tuhuma za msingi na yeye aruhusiwe kuendelea na upelelezi na baadaye mashitaka.

(7) Majaji wa kitengo cha usikilizaji wa awali watatathimini kama maombi yaliyoletwa ni ya msingi; kama ni ya msingi wataruhusu upelelezi uendelee.

(8) Mwendesha Mashitaka akikamilisha upelelezi wake, ataomba Mahakama kutoa amri ya kukamatwa mtuhumiwa au samansi. Kabla kesi haijaanza kusikilizwa, mtuhumiwa anahitajika kufika Mahakamani ili Majaji wathibitishe kama anayo kesi ya msingi kuendelea na usikilizwaji ama la.

(9) Endapo mtuhumiwa atakuwa mkaidi, baada ya maombi huweza kutolewa amri ya kumkamata na kumfikisha Mahakamani. Nchi wanachama watawajibika kushirikiana katika kukamata na kumpeleka huko. Lakini kama mtuhumiwa sio mkaidi, hutolewa samansi ya kumwita afika Mahakamani kwa hiari yake.

(10) **Mtuhumiwa kufika Mahakamani -** Mtuhumiwa akitokea Mahakamani kwa mara ya kwanza (*iwe amefika kwa kukamatwa kwa amri ya Mahakama au kwa samasi akaja kwa hiari yake bila kukamatwa*), Majaji watatu (3) wa kitengo cha usikilizwaji wa kabla (Pre-Trial Chamber) wataendesha shauri la kuthibitisha tuhuma za msingi. Kuthibitisha tuhuma ni kujiridhisha kama tuhuma ina mashiko na inastahili kuendelea na usikilizwaji kamili. Katika kufanya hivyo watahakikisha mtuhumiwa anaelewa tuhuma yake kwa lugha itakayomfanya aelewe tuhuma na kila kinachoendelea katika mwenendo wa mashitaka.

KUTHIBITISHA KAMA KUNA KOSA LA MSINGI ILI KUENDELEA NA USIKILIZWAJI (confirmation of charges)

Mwendesha Mashitaka akikusanya ushahidi unaotosheleza kuendelea na usikilizwaji wa kesi, usikilizwaji huo hautaanza hadi Kitengo cha Kabla ya usikilizwaji (Pre-Trial Chamber) kitathimini na kuamua kama yapo mashitaka ya msingi kuruhusu usikilizwaji kamili uendelee. Hii inalinda haki ya mtuhumiwa kupotezewa muda kwa mashitaka yasiyo na mashiko, na kwa Mahakama kuendesha kesi isiyo na mashiko. Kitengo hiki kinatarajiwa kutathimini hoja zitakazowakilishwa na na pande zote na kutoa maamuzi ya kuthibitisha kama kuna kesi ya msingi kuruhusu usikilizwaji ama la.

Wakati hatua hii inaendelea, Mwendesha Mashitaka anaweza kuendelea na upelelezi na anaruhusiwa hata kurekebisha mashitaka yaliyowasilishwa (atatakiwa pia kumpa mtuhumiwa taarifa ya kurekebisha mashitaka hayo). Vilevile, anaweza kuondoa shitaka kwa kupeleka taarifa kitengo cha kabla ya usikilizwaji, akieleza sababu za msingi zilizopelekea aombe kuondoa mashitaka.

Kwa mujibu wa ***Ibara ya 61*** ya sheria ya ICC utaratibu katika kuthibitisha mashitaka ni kama ifuatavyo: -

1. Baada ya mtuhumiwa kufikishwa Mahakamani kwa kukamatwa au kwa hiari yake mwenyewe, Kitengo cha Usikilizwaji wa awali (Pre-Trial Chamber) chenye jopo la Majaji watatu (3) kitaendesha shauri la kutathimini na kuthibitisha mashitaka ya msingi, wakiwepo ***Mwendesha Mashitaka, Mtuhumiwa*** pamoja na ***Wakili wake***. Usikilizaji unaweza kuendelea bila uwepo wa mtuhumiwa kama atakuwa ameridhia (***ibara ya 61 ya Sheria ya ICC***), au kama amekimbia hapatikani na hatua za msingi kumjulisha

uwepo wa shauriii au kumfikisha Mahakamani zimefanyika bila mafanikio. Katika mazingira ya mtuhumiwa kutokuwepo, Mahakama inaweza kuruhusu awakilishwe na Wakili kwa maslahi ya haki.

2. Katika muda wa kutosha, mtuhumiwa atapewa hati ya mashitaka na ataambiwa ushahidi ambao Mwendesha Mashitaka anatarajia kuuleta dhidi yake. Mahakama pia inaweza kutoa amri ya kufichua taarifa kwa usikilizaji wa kesi.

3. Mwendesha Mashitaka ataleta hoja za kiushahidi kujenga viini vya mashitaka aliyoyaleta dhidi ya mtuhumiwa, ushahidi unaoweza kuwa wa nyaraka au wa Muhtasari tu. Katika hatua hii sio lazima alete mashahidi wanaotarajiwa kuitwa wakati wa usikilizwaji kamili.

4. Wawakilishi wa waathirika wa kosa pia huwa wanapewa nafasi kuwasilisha maoni na fikra za waathirika.

5. Mtuhumiwa anayo nafasi kupinga mashitaka, au ushahidi ulioletwa dhidi yake katika hatua hii na anayo haki kuleta ushahidi wake kinzani.

6. Jopo la Majaji hao watatu (3) wa Kitengo cha Awali, ndani ya siku sitini (60), watatathimini kama ushahidi unajitosheleza kuilazimu Mahakama kwenda hatua inayofuata ya usikilizwaji kamili wa kesi na watatoa maamuzi ***kama mashitaka ya msingi yameundwa au la***.

   - Endapo ushahidi utaunda mashitaka ya msingi, mashitaka yatathibitishwa na mtuhumiwa atapelekwa Kitengo cha Usikilizwaji kamili kujibu makosa yale tu yaliyothibitishwa na Kitengo cha Usikilizwaji wa Kabla.

   - Kama ushahidi hauundi mashitaka ya msingi, Kitengo hakitathibitisha uwepo wa mashitaka ya msingi, na aidha kinaweza kuahirisha kesi na kumwomba Mwendesha Mashitaka kuleta ushahidi wa ziada au kufanya upelelezi zaidi, au kumwomba Mwendesha Mashitaka arekebisha mashitaka aliyoyaleta kwasababu ushahidi umeonyesha uwepo wa makosa mengine tofauti na yale aliyoyapendekeza. Mahakama ikikataa kuthibitisha uwepo wa mashitaka, Mwendesha Mashitaka hazuiliwi hapo mbeleni kuleta tena maombi ya uthibitishwaji kama maombi hayo yataungwa mkono na ushahidi.

7. Inawezekana kukawa na uhitaji kurekebisha hati baada ya uthibitishwaji kitengo cha ***Usikilizwaji wa Kabla*** kufanyika; Mwendesha Mashitaka anaruhusiwa kurekebisha hati ya mashitaka yenye makosa ambayo tayari yameshathibitishwa, lakini endapo kuna nyongeza ya makosa mapya, au anataka kubadilisha na mashitaka mazito zaidi, kutatakiwa kufanyika usikilizwaji mpya wa kuthibitisha makosa hayo.

8. Hatua inayofuata baada ya mashitaka kuthibitishwa, ni Ofisi ya Rais wa Mahakama kuunda kitengo cha usikilizwaji kamili (Trial Chamber), bila kuathiri aya ya 9 ya ibara hii, na ibara ya 64(4), kitakachokuwa na wajibu kuendesha usikilizwaji wa kesi na hata kufanya majukumu ambayo yangefanywa na kitengo Cha usikilizwaji wa Awali kama yatahitajika kufanyika kwenye mwenendo wa usikilizwaji.

9. Katika hatua ya usikilizwaji kamili, kwa ridhaa ya Mahakama, Mwendesha Mashitaka anaweza kuondoa mashitaka. Hati yeyote ya ukamataji itakoma kuwa na nguvu kwenye makosa yeyote ambayo hayajathibitishwa na Kitengo cha Usikilizwaji wa Awali au yaliyoondolewa na Mwendesha Mashitaka.

Hatua ya Usikilizwaji Kamili

Katika hatua ya usikilizwaji inahusisha koramu ya Majaji watatu na yafuatayo huzingatiwa: -

1. Mwendesha Mashitaka lazima athibitishe pasi na kuacha shaka tuhuma dhidi ya mshitakiwa, kwa kuwakilisha ushahidi utakaothibitisha viini vya kosa husika. Ushahidi huu kama ulivyo utaratibu utatikishwa na hoja kinzani toka upande wa utetezi ili kuonyesha kama ni wa kweli.

2. Utetezi wa upande wa mtuhumiwa utazingatiwa, ambao utahusisha pia ushahidi wa mashahidi wake kama wapo.

3. Majaji watatoa hukumu

4. Upande wowote usioridhika waweza kukata rufaa.

MCHANGANUO WA AINA YA MAKOSA NA VIINI VYAKE CHINI YA MAHAKAMA YA ICC NA VIINI VYAKE

1) Makosa ya Kimbari (Genocide)

*Kosa la **Kimbari** linakuwa limetendeka kama mtu atatenda vitendo vilivyozuiliwa na **ibara ya 6(a) – (e)** vya Sheria ya ICC huku akiwa na uelewa na nia ya kuteketeza/kuangamiza kwa ujumla au kwa kiwango fulani kundi la watu wa taifa,kabila,rangi au dini fulani, dhamira ikilenga aina ya watu wa kundi hilo wasiendelee kuwepo/wafutike/wapotee.*[9]

Msingi mkuu wa kosa hili ni kuteketeza kundi fulani la watu wasiendelee kuwepo na ushahidi wa kosa lazima uunde viini vyenye minajiri hiyo.[10] Viini vinavyounda kosa la kimbari katika kuthibitisha vitendo vilivyozuiwa na ***ibara ya 6(a) – (e***) ni: -

*(1) Ithibitike kwamba mtuhumiwa ametenda vitendo vilivyozuiliwa vilivyoorodheshwa katika ibara ya 6(a)-(e) ya Sheria ya ICC (**actus reus**).*

*(2) Nia iwe ni kuteketeza kwa ujumla au kwa kiwango fulani kundi husika la watu iwe la kitaifa, kabila, rangi au dini (**mens rea**).*

(3) Ushahidi uthibitishe kwamba Mwathirika anatoka kundi fulani la utaifa, kabila, rangi au dini na ambali lililolengwa. Mtu anashambuliwa kwa sababu tu anatoka kundi fulani la watu wa taifa, kabila, rangi au dini.[11]

Mara zote ukiona neno "**kuteketeza/kuangamiza kundi**" katika kosa hili, inaashiria kwamba mlengwa katika kosa hili sio mtu/watu binafsi, bali ni kundi, hili ni **kosa dhidi ya kundi** na linakuwa limetimia hata kama mkosaji amedhuru mtu mmoja tu, maadamu nia iliyokuwepo akilini mwake ililenga kuteketeza kundi, tayari ameshatimiza kosa. Tabia kuu inayolitambulisha na kulitofautisha kosa hili na mengine, ni nia ya mkosaji; sio tu ya kudhuru mtu/watu au kuua mtu/watu, bali "**kuteketeza kundi la watu fulani ili wasiendelee kuwepo**".

Wakati wa Mauaji ya Kimbari Rwanda 1994, pamoja na uwepo wa Mkataba unaohusu Makosa ya Kimbari (Genocide Convention 1948) jumuiya ya kimataifa kwa uzembe, kwa kutojali au kwa makusudi, awali ilijifanya

---

[9] Maana ya "mauaji ya kimbari" angalia kesi ya **Aloys Simba**, Case No. Ictr-01-76-A, Appeal Judgement, 27 Nov. 2007, 266; na kesi ya **Clément Kayishema et al**., Case No. ICTR-95-I-A, Appeal Judgement, 1 June 2001, 91.

[10] **Schabas, W.A., Genocide in International Law** – The Crime of Crimes, Second edition, Cambridge: Cambridge University Press, 2009

[11] **Prosecutor v. Rutaganda**, Case No. ICTR-96-3-T, Judgment, Trial Chamber, 6 December 1999, para. 56. Pia angalia kesi ya **Prosecutor v. Akayesu**, op. cit. note 272, para. 514. Na kesi ya **Prosecutor v. Kayishema and Ruzindana,** Case No. ICTR-95-1-T,21 May 1999, para. 98., kesi ya **Prosecutor v. Jelisic**, Case No. IT-95-10, 14 December 1999, para. 70.

kutotambua mauaji ya Rwanda kama yalikuwa ya kimbaru au la. Maafisa wengi wa Marekani walipohojiwa kwa kile kilichokuwa kinaendelea walisema sio mauaji ya kimbari, pengine hawakujisumbua kutafiti maana halisi ya mauaji yakimbari kulingana na ushahidi wa wazi kwa matendo yaliyokuwa yakiendelea mtaani.

Katika ibara ya 6(a)-(e) matendo yanayokatazwa na ambayo ndiyo yanaunda kosa la Kimbari ni kama yafuatayo:-[12]

(a) **Kuua watu wa kundi fulani.** Ithibitike kwamba, mtuhumiwa aliua mtu mmoja au zaidi, wanaotoka kundi fulani la taifa, kabila, rangi au dini akiwa na nia ya kuteketeza kwa ujumla au kwa kiwango fulani kundi hilo, na tukio lilikuwa wazi likilenga kuteketeza au lingeweka mazingira ya watu wa kundi hilo kuteketea/kufutika. **Mfano**; mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi wa Rwanda 1994. Wauaji walikuwa na nia ya kuteketeza Watutsi wafutike wasiendelee kuwepo Rwanda (ili Rwanda kusiwe na Watutsi). Ili kuthibitisha kipengele hiki, ni lazima ushahidi uonyeshe wazi kwamba mkosaji ameua mtu mmoja au zaidi wanaotoka kundi fulani la kitaifa, kabila, rangi au dini huku akiwa na nia na uelewa, na matendo yake hayo yaonyeshe wazi alilenga kundi hilo mahsusi kwamba liteketee.

(b) **Kusababisha madhara makubwa kimwili au kiakili** kwa watu wa kundi fulani la kitaifa, kikabila, rangi au dini. Utatakiwa kuletwa ushahidi kwamba mtuhumiwa alisababisha madhara makubwa ya kimwili au kiakili kwa mtu mmoja au zaidi, wanaotoka kundi fulani la taifa, kabila, rangi au dini akilenga kwa kufanya hivyo angewateketeza kundi hilo kwa ujumla au kwa kiwango fulani.

(c) **Kwa makusudi, kuwaweka watu kwenye mazingira hatarishi yatakayosababisha wateketee/wafutike**. Ushahidi lazima uonyeshe mtuhumiwa aliweka mazingira fulani kwa mtu mmoja au zaidi wanaotoka kundi fulani la kitaifa, kikabila, rangi au dini, akiwa na nia ya kuteketeza kundi lao kiujumla au kwa kiwango fulani na matendo yake yanadhihirisha hivyo. **Mfano**; kufukuzia watu wa kundi fulani kwenye barafu akijua watakufa kwa baridi kali, kwenye hatari ya magonjwa mfano Ebola, kwenye eneo la vita, kwenye mazingira ya njaa wakose chakula wafe, kwenye mazingira yeyote ambayo yatawafanya watu wa kundi hilo wateketee na aina yao ipotee isiendelee kuwepo n.k, kiujumla

[12]**Georges A. N. Rutaganda**, Case No. ICTR-96-3-T, Trial Judgement, 6 Dec. 1999, 59. ...AS STATED BY ICTR TRIAL at the above case at page 60 THAT [F]or any of the acts charged to constitute genocide, the said acts must have been committed against one or more persons because such person or persons were members of a specific group, and specifically, because of their membership in this group. Thus, the victim is singled out not by reason of his individual identity, but rather on account of his being a member of a national, ethnical, racial or religious group. The victim of the act is, therefore, a member of a given group selected as such, which, ultimately, means the victim of the crime of genocide is the group itself and not the individual alone. The perpetration of the act charged, therefore, extends to encompass the realization of the ulterior purpose to destroy, in whole or in part, the group of which the person is only a member.)

au kwa kiwango fulani). Nia iwe ni kuteketeza watu wa kundi hilo kiujuma au kwa kiwango fulani.

(d) **Kupanga njama za kuzuia watu wa kundi fulani wasizaliane.** Ushahidikuthibitisha kosa hili uonyeshe mtuhumiwa alielekeza njia za kuua kizazi kwa mtu mmoja au zaidi wanaotoka kwenye kundi lengwa la kitaifa, kikabila, rangi au dini kwa kufanya hivyo akiwa na uelewa na nia ya kuteketeza watu wa kundi husika kwa ujumla au kwa kiwango fulani na ionekane wazi matendo yake yalikuwa yanalenga wasizaliane ili aina ya watu wa kundi hilo ifutike/wateketee kiujumla au kwa kiwango fulani.

(e) **Kwa kutumia nguvu, kuhamisha watoto wa kundi fulani hadi mahali kwingine kwenye kundi lingine**. Ushahidi uonyeshe mkosaji alihamisha mtu mmoja au zaidi walioko chini ya miaka 18 huku akijua umri wao, wa kundi fulani la watu wa kitaifa, kabila, rangi au dini huku akiwa na uelewa na nia kwamba kwa kufanya hivyo ataliteketeza kundi hilo kwa ujumla au kwa kiwango fulani ili lisiendelee kuwepo.

KUMBUKA: *Haya yote yatakuwa kosa la kimbari kama mkosaji alifanya hivyo akiwa na nia na uelewa kwamba anawalenga watu wa kundi hilo ili wateketee wasiendelee kuwepo. Sio kila mauaji au matendo maovu ni kosa la kimbari, kuunda kosa ni lazima viini vya kosa vionekane vikilenga kuteketeza watu wa kundi husika kwa ujumla au kwa kiwango fulani.*[13]

Mfano: Dunia nzima hakuna mtu anayebisha uwepo wa mauaji ya Kimbari Rwanda 1994 ambapo watu wa kabila la Wahutu walidhamiria kuteketeza kabila la Watutsi ili wafutike/wateketee/wasiendelee kuwepo Rwanda. Mfano mwingine ni pale MANAZI wa Ujerumani walipodhamiria kuwateketeza Wayahudi wote wa wa maeneo yao ili aina ya watu wa kundi la wayahudi ifutike/ipotee. Vilevile, Mauaji ya Bosnia pia, Waserbia walikuwa wamedhamiria kuwateketeza Waislam au watu wa Bosnia na Hezegovina wasiendelee kuwepo eneo lile.

Ukiangalia kwa makini, utaona ni dhahidi matendo haya hayakulenga mtu mmoja, yalilenga kundi fulani la watu na huu ndio utofauti wa makossa ya Kimbari na makossa mengine. Ukiangalia ukatili unaofanywa katika kosa hili ni kuteketeza kuanzia kitoto kichanga, vijana, wazee hadi vikongwe; wahalifu hulenga kuteketeza kila mwanadamu anayetoka kundi husika.

Mauaji ya kimbari hayaji kwa bahati mbaya, wala ghafla, huja polepole; hurutubishwa na virutubishi mbalimbali, yanapangwa kwa kipindi kirefu na kwa ustadi kiasi kwamba kama jamii ipo makini itatambua dalili zake na

[13] Kuhusu nia ya kuteketeza katika mauaji ya kimbari, angalia kesi ya **Radislav Krstid,** Case No. IT-98-33-A, Trial Judgement, 2 Aug. 2001, 590; na Krstid, Aappeal Judgment No. 19, 22. na **Radislav Krstid**, Case No. IT-98-33-A, Appeal Judgement, 19 April 2004, 25. Mahakama ya ICTY

kuyazuia. Hii ni muhimu kujua ili kuzuia pindi viashiria vionekanapo. Viashiria vyake huanza kitambo kabla, mfano; kusambaza chuki katika jamii dhidi ya kundi fulani, kuhamasisha mashambulizi dhidi ya watu fulani, kugawanya watu kikabila, kidini au kitaifa n.k na mwishowe baada ya watu kugawanyika na kuchukiana kabisa, huweza kuwa wakatili kupindukia dhidi ya kundi lingine hata kuamini wengine hawana haki ya kuendelea kuwepo. Ndivyo ilivyotokea Rwanda mwaka 1994 baada ya chuki na mgawanyiko kuenea kwa njia mbalimbali, wanasiasa kupandikiza chuki kwa raia hadi kufika kipindi raia aliona jirani yake ambaye ni Mtutsi ni sawa na mnyama tu anayestahili kuuawa na kuteketezwa asiendelee kuwepo Rwanda.

2) Kosa la Uhalifu dhidi ya Ubinadamu (Crimes against Humanity)

Uhalifu dhidi ya ubinadamu ni matendo yeyote yanayozuiwa katika **ibara ya 7(a)-(k)** ya Sheria ya Mahakama ya ICC, kama yatakuwa yametendeka kama **"shambulizi lililoenea (la halaiki/kusambaa) au lililopangiliwa dhidi ya raia";** na wakati huo mkosaji au yule anayezembea hadi hayo yakatokea awe na uelewa kuwa shambulio hilo linafanywa dhidi ya raia.[14]

Mazingira yanaweza kuonyesha kama shambulio fulani lilikuwa la "**kuenea (halaiki/kusambaa) kwa raia**" au **lililopangiliwa dhidi ya raia**" kutokana na ushahidi wa kimazingira; Kwa mfano, shambulio lililoenea (widespread) litatambulika hivyo kutokana na ukubwa wa eneo lililoathirika au idadi ya raia waliodhurika. Pia hii inaweza kujumuisha mashambulio makubwa yanayofanywa mara kwa mara, yanayojirudiarudia kwa tabia zilezile, ya eneo kubwa, yasiyo na uchaguzi kati ya raia na wapiganaji, yanayorushwa bila uchaguzi eneo linalojulikana kuwa ni makazi ya raia, yanayojumuisha kila mtu na yaliyoathiri watu idadi fulani ambayo sio ya kawaida kuhalalisha kilichotokea. Ili lionekane lilipangiliwa linaweza kuwa la kujirudiarudia kwa tabia zilezile.[15] Ni lazima lionekane lilikuwa ni mpango au sera ya Serikali au kundi fulani dhidi ya raia wema.[16]

Tukisoma ***ibara ya 7 (a)-(k),*** miongoni mwa matendo yanayozuiwa yanayounda kosa hili kama yatakuwa yametendeka kama moja ya "***shambulio la kuenea/halaiki*** au "***lililopangiliwa***" dhidi ya raia, ni kama yafuatayo: -

(a) **Mauaji ya kukusudia**. Lazima ushahidi uonyeshe mtuhumiwa aliua mtu mmoja au zaidi katika shambulio lililoenea/sambaa au lililopangiliwa

[14]**Prosecutor v Semanza**, Case No. ICTR-97-20 (Trial Chamber), May 15, 2003. para 326.

[15]**Situation in the Republic of Kenya**, Decision Pursuant to Article 15 of the Rome Statute, 89 (fn 81), 92 citing **Tihomir Blaškid**, Case No. IT-95-14-T, Trial Judgement, 3 March 2000, 205. Pia angalia kesi ya "**Jean Paul Akayesu**, Trial Judgement pg. 580 pia angalia **Blaškid**, Appeal Judgment pg.101; na **Kunarac et al.**, Appeal Judgment pg.93-96; Radoslav Brđanin, Case No. IT-99-36-T, Trial Judgement, 1 "

[16]**Prosecutor v Bagilishema**, Case No. ICTR-95-1A-T (Trial Chamber), June 7, 2001. para. 80

dhidi ya raia, na alijua kuwa tukio lilingekuwa la kuendea kwa raia au lilikuwa sera iliyopangwa dhidi ya raia wema. ***Sio lazima mwili uonekane*** kuthibitisha pasi na shaka kuwa kifo kimetokea, ushahidi wa kimazingira unaweza kuthibitisha kifo hata kama mwili hauonekani.[17]

(b) **Uteketezaji raia au mauaji ya watu idadi kubwa** (extermination or mass killing). Kuua watu idadi kubwa/ambayo sio ya kawaida na katika eneo lenye ukubwa fulani.[18]Hii pia inajumuisha kuwaweka watu katika mazingira yatakayowasababishia maafa. Mfano; kuwafukuzia watu kwenye eneo lenye mlipuko wa magonjwa, kuwafukuzia watu eneo la barafu na hakuna namna za kujisitiri n.k.

(c) **Kufanya utumwa**. Hii inajumusha uwepo wa nguvu ya watu fulani kumiliki binadamu wengine kama mali, kuuza, kununia, kuazimisha, vitendo vya kudhibiti uhuru wa mtu anayesemekana kuwa mtumwa kisaikolojia, kimwili, namna anavyomzuia asitoroke au asiwe na uhuru kutembea, matumizi ya nguvu dhidi yake, mateso, kutumikishwa kingono na kikazi na kitambo alichommiliki. Hivyo vyote ni kipimo cha ushahidi wa kimazingira kuunda kosa.[19]

(d) **Kuhamishwa au kuhamisha raia wema kinguvu**. Hii inajumuisha kuondoa watu toka kwenye makazi yao ya kudumu kwa kuwafukuza au kwa kutumia nguvu ya aina yeyote ile. Katika kuthibitisha kosa hili, kuhamisha/kufukuza watu lazima kuwe kinyume na sheria, mfano, ***Geneva Convetion IV Article 49 and AP II Article 17*** inaruhusu kuhamisha idadi fulani ya raia kama usalama wao utakuwa hatarini, pamoja na kwamba baada ya usalama kurudi ni lazima warudishwe kwenye makazi yao. Mtuhumiwa lazima awe alikuwa na uelewa kuwa kufanya hivyo ni sera ya iliyopangiliwa au ya halaiki kwa raia wema.

(e) **Kufunga raia jela bila sababu ya msingi** au namna nyingine za kunyang'anya haki ya uhuru kwa hali ya juu - ***Imprisonment or other severe deprivation of physical liberty***(*kama hayo yanafanywa kama miongoni mwa shambulio lililoenea au lililopangiliwa kwa raia wema*). Hili linaweza kuthibitishwa kama raia mwema katika kufungwa huko, hakuna sababu ya msingi kisheria yeye kufungwa na hakuna hatua zozote za kisheria zinazoendelea katika vyombo vya kutoa haki na mtenda kosa hilo anaelewa kwamba kufanya hivyo kutamwondolea haki ya uhuru mwathirika.[20] Hata hivyo, hii haijumuishi kukamatwa kwa sababu

---

[17]**Moinina Fofana et al**. (CDF Case), Case No. SCSL-2003-11-T, Trial Judgement, 2 Aug. 2007, 144, citing Krnojelac, Trial Judgment, 326, na Brđanin, Trial Judgment 385

[18]**Kayishema,** Trial Judgment 145.

[19]**Kunarac et al**., Trial Judgment 542 and Appeal Judgement 119-121, 356.

[20]**Rome Statute**, Art. 7.

za msingi na kufunguliwa mashitaka au kufungwa au kukamatwa na kufukuzwa nchini kwa mujibu wa sheria za nchi.

(f) **Mateso kwa raia wema**. Hii inajumuisha matendo yanayosababisha maumivu makali yanayofanywa kwa makusudi dhidi ya raia walio kizuizini, kiakili, na kimwili kinyume na sheria. Mateso yanaweza kuwa yanalenga kupata taarifa fulani, kuadhibu, kutishia, kunyanyasa au kulazimisha mteswaji kufanya jambo fulani yeye mwenyewe au mtu wake wa karibu. Yanaweza kujumuisha vipigo, kung'oa meno au kucha, kuchoma moto, kushitua kwa umeme, kutoruhusu mapumziko, kutopewa chakula kwa muda mrefu, kuwekwa mazingira machafu ili yamdhuru mteswaji, kutopatia tiba, kuua ndugu wa mteswaji, ubakaji, vitisho vya kijinsia,n.k [21] yote haya yanatakiwa yawe yamefanywa kwa mpangilio "au" kwa kuenea dhidi ya raia, ndio uhalifu dhidi ya ubinadamu litakuwa limetendeka.[22] Kama ilivyo kawaida, msingi wa kosa uwe ni shambulio dhidi lililoenea kwa watu hao na lililopangiliwa, huku mtuhumiwa akiwa na uelewa huo wakati wa kutenda kosa.

(g) **Ubakaji.** Ushahidi uonyeshe mtuhumiwa alimwingilia kimwili raia kwa nguvu au vitisho bila ridhaa yake, na vitendo hivyo vilifanyika kama mojawapo ya mashambulizi yaliyoenea na yaliyopangwa dhidi ya raia. **Kundi hili linahusisha vitendo vya utumwa wa ngono, kulazimisha** raia kuwa makahaba, kulazimisha raia kubeba mimba, kulazimisha raia kuondoa vizazi vyao au tendo lolote la uchokozi wa kingono wa uzito fulani.[23]

(h) **Manyanyaso dhidi ya kundi fulani** linalotambulika kidini, kirangi, kitaifa, kikabila, kisiasa, kiutamaduni au kijinsia. Unyanyasaji huo uwe ulilenga kisiasa, rangi, utaifa, kabila, tamaduni, dini, jinsia au misingi mingine inayotambulika kimataifa kutoruhusiwa na sheria za kimataifa. Vitendo hivi vinatakuwa kuwa vimefanywa kama moja ya shambulizi kwa raia lililoenea au lililopangiliwa na mtuhumiwa awe alikuwa na uelewa huo.

(i) **Raia kupotezwa** (***enforced disappearance of persons***).[24] Ushahidi uonyeshe mtuhumiwa alikamata, aliweka kizuizini au aliteka mtu mmoja

---

[21]See, e.g., **Čelebidi,** Trial Judgment 461-469**; Furundžija**, Appeal Judgment 113.
[22]**Milan Milutinovid et al**. ("Šainovid et al.".), Case No. IT-05-87-T, Trial Judgement, 26 Feb. 2009, 194 – 201.
[23]**Kunarac et al**., AJ 127; Stakid, TJ 755; **Gacumbitsi**, AJ 147-157. ICC Elements of Crimes, Art. 7(1)(g)-1(1), Art. 7(1)(g)-2(2). Of the ICC Statute.

[24] Angalia ibara ya 1 ya "***International Convention for the Protection of All Persons from Enforced Disappearance***" ikifafanuliwa na ***ibara ya 2*** ya Mkataba huo inasema " *For the purposes of this Convention, "**enforced disappearance**" is considered to be the arrest, detention, abduction or any other form of deprivation of liberty by agents of the State or by persons or groups of persons acting with the authorization, support or acquiescence of the State, followed by a refusal to acknowledge the deprivation of liberty or by concealment of the fate or whereabouts of the disappeared person, which place such a person outside the protection of the law*",

au zaidi au alikataa kukubali kwamba alimkamata,alimweka kizuizini, alimteka au kutoa taarifa za hatima yake au wapi alipo. Kukamata, kuweka kizuizini au kuteka huko kulifuatiwa au kuliambatana na kukataa kukiri kunyang'anya haki ya uhuru au kutoa taarifa za hatima au wapi walipo watu hao, au, kukataa huko kumeambatana na kunyang'anya haki ya uhuru wa mtu. **Ushahidi uonyeshe matendo hayo yalifanyika kwa ruhusa au kwa kuungwa mkono na Serikali au kundi la kisiasa**, na mtuhumiwa awe alilenga kumwondoa mtu au watu hao toka kwenye ulinzi wa sheria kwa muda mrefu. Matendo haya pia yanatakiwa yawe yametendeka kama moja ya shambulio lililoenea au lililopangiliwa dhidi ya raia wema. Hata hivyo, kutokana na mkanganyiko wa viini vya kosa hili, litatambulika kama limetendwa na watu zaidi ya mmoja wanaoshirikana kutenda kosa. Pia, neno "kuwekwa kizuizini – detained" inajumuisha watuhumiwa wenye kizuizi na yapo mazingira ambayo mtu anaweza kuwa aliwekwa kizuizini kwa mujibu wa sheria.

(j) **Ubaguzi wa rangi - apartheid**. ushahidi uonyeshe kwamba, mtuhumiwa ametenda kosa lisilo la ubinadamu kwa mtu mmoja au zaidi, tendo hilo likiwa la unyanyasaji na kiutawala wa kundi la rangi moja dhidi ya watu toka makundi mengine ya rangi akiwa na nia ya kuendeleza mfumo huo wa kibaguzi na vitendo hivyo vikiwa vinafanywa kwa kusambaa kwa raia na kwa mpangilio.

(k) **Matendo mengine yaliyo kinyume na ubinadamu** yanayofanana na hayo yanayofanywa kwa makusudi ya kusababisha mateso makubwa au maumivu makubwa ya mwili au ya kiakili dhidi ya raia.

Tofauti kati ya kosa hili na lile la *kimbari* ni kwamba, kosa la *kimbari* ni kosa dhidi ya kundi, wakati *uhalifu dhidi ya ubinadamu* ni kosa dhidi ya raia ambao hawapo kwenye mapigano. Ukimbari unakuja pale panapokuwa na ***shambulio linalolenga kuteketeza kundi la watu fulani, liwe la kidini, kitaifa, kabila n.k, kwa nia ya kuteketeza aina ya watu wale wasiwepo kabisa***, wakati uhalifu dhidi ya ubinadamu ni makosa yeyote yaliyotendeka dhidi ya raia wasio kwenye mapigano endapo tu yalikuwa yameenea au yamepangiliwa.

Kwa maana hiyo, kosa la kimbari limeundwa ili kuzuia kuteketeza makundi ya watu (kabila, dini, taifa n.k), na uhalifu dhidi ya ubinadamu limeundwa ili kuzuia mashambulizi yasiyo na sababu ya halaiki/kuenea au yaliyopangiliwa dhidi ya raia wema.

---

pia angalia "***Office of the United Nations High Commissioner for Human Rights, Enforced or Involuntary Disappearances, act Sheet No. 6/Rev.3 - pg.11***"

"**Shambulio**" katika uhalifu dhidi ya ubinadamu linaweza kutendeka wakati wa vita au wakati wa amani, haihitaji kuwa na vita au machafuko; [25]kosa hili pia linaweza kutendeka kwa njia ya mateso kwa raia.[26] Pia, "**shambulio**" husika ni "**lazima lilenge raia na mshambuliaji awe na uelewa huo wakati wa kushambulia**"; makazi ya raia maana yake ni makazi ya watu ambao hawajihusishi na mapigano (raia wema).[27]

Na ili kosa hili likamilike sio lazima wakazi wote wa eneo lililoshambuliwa wadhurike au washambuliwe, hata kushambulia eneo dogo tu lakini watu fulani wakadhurika, inaunda kosa. Ni lazima wawepo watu kadhaa waliodhurika ili kuishawishi Mahakama kuwa kosa hilo lilikuwa kubwa lililoenea au lililopangwa dhidi ya raia.[28] Kama tulivyokwishaona, dhima ya kosa hili ni kuzuia makundi maalumu au hata Serikali za mataifa mbalimbali duniani kushambulia raia wema ambao hawajihusishi na mapigano.[29]

USHAHIDI WA KIMAZINGIRA: ushahidi wa kimazingira ili kuonyesha kosa limefanyika huangaliwa aina na njia shambulizi lilivyofanyika, idadi ya watu waliodhurika, hali ya waathirika, kubagua/kuchagua maeneo aliyoshambulia (kwanini ameshambulia pale na sio kwingine), aina ya makosa yaliyotokea (maafa,mateso n.k), upinzani toka kwa washambuliaji, njia zozote zilizochukuliwa kukinga raia wasidhurike, lengo la kushambulia eneo husika ni nini?, matokeo ya shambulio, mlingano kati ya matendo ya mwathirika na uzito wa shambulizi, muda shambulizi lilivyofanyika na mfanano wa matendo ya mshambuliaji na nia ya kushambulia kwenyewe .[30]

---

[25] Isipokuwa kwa ICTY ambako uhalifu dhidi ya ubinadamu lazima lifanyike katika mazingira ya vita , Mahakama ya ICTR na ICC inatambua shambulio lolote dhidi ya raia kuwa ni uhalifu dhidi ya ubinadamu (crime against humanity).

[26]**Dragoljub Kunarac et al**., Case No. IT-96-23-A, Appeal Judgement, 12 June 2002, 86. Na **Prosecutor v. Jean Paul Akayesu**, TJ 676 – 684.

[27] Soma "Article 50 of Additional Protocol I to the Geneva Conventions (AP I)" kujua raia wema ni nani.
[28]Tihomir Blaškid, Case No. IT-95-14-A, Appeal Judgement, 29 July 2004, 106, kesi ya Kunarac et al., AJ 91. Na kesi ya **Duško Tadid, Case No. IT-94-1-T**, Trial Judgement, 7 May 1997, 644.

[29]**Clément Kayishema et al**., Case No. ICTR-95-I-T, Trial Judgement, 21 May 1999, 122. Mrkšid, Appeal Jjudgment pg 41; Krnojelac, TJ 127, Mrkšid, AJ 41; **Kunarac** et al., Appeal Judgment 100.

[30] Moinina Fofana et al., Case No. SCSL-2003-11-A, Appeal Judgement, 28 May 2008, 247, pia angalia "Geneva Conventions 1949 (adopted 12 Aug. 1949, entered into force 21 Oct. 1950) (GC I-IV), Common Art. 3, and Additional Protocol I (adopted 8 June 1977, entered into force 7 Dec. 1978) (AP I) Arts. 43 and 50; Situation in the **Republic of Kenya, Case No. ICC-01/09**, Decision Pursuant to Article 15 of the Rome Statute on the Authorization of an Investigation into the **Situation in the Republic of Kenya**, 31 March 2010, 82 (fn 74), citing Jean-Pierre Bemba Gombo, Case No. ICC-01/05-01/08-424, Decision Pursuant to Article 61(7)(a) and (b) of the Rome Statute on the Charges of the Prosecutor Against Jean-Pierre Bemba Gombo, Pre-Trial Chamber II, 15 June 2009,78; Kunarac et al., TJ 425. **Situation in the Republic of Kenya**, Decision Pursuant to Article 15 of the Rome Statute, 82(fn 73), citing Bemba Confirmation Decision 77; Kunarac et al., AJ 91-2; Milomir Stakid, Case No. IT-97-24-T, Trial Judgement, 31 July 2003, 624; **Mitar Vasiljevid**, Case No. IT-98-32-T, Trial Judgement, 29 Nov. 2002, 33. , pia angalia **Kordid e**t al., AJ 50; Stanislav Galid, Case No. IT-98-29-A, Appeal Judgement, 30 Nov. 2006, 136 – 137, fn 437; See **Vidoje Blagojevid** et al., Case No. IT-02-60-T, Trial

3) Makosa ya Kivita (War Crimes)

Kwa mujibu wa ***Ibara ya 8 ya Sheria ya Mahakama ya ICC***, na kama lilivyo jina lake, haya ni Makosa yanayotokea wakati na katika mazingira ya kivita tu. Katika mazingira ya kivita, zipo Sheria za Kimataifa zilizowekwa kufuatwa katika uwanja wa vita, na yeyote anayekiuka Sheria hizo ndiye anayekuwa ametenda Makosa ya kivita. ***Ibara ya 8(2)(a***) ya Sheria ya ICC inayatambua Makosa ya Kivita kuwa ni ukiukwaji wa kiwango cha juu wa ***Mikataba ya Geneva ya Agost 12, 1949*** dhidi ya watu au vitu vinavyolindwa na mikataba hiyo.

Mara nyingi kupigana vita kuna madhara makubwa kwa pande zinazopigana na kwa raia; hata hivyo, sio kupigana vita kote ni kubaya au kunakatazwa, wakati mwingine vita ni ya muhimu ili kuokoa maslahi fulani ya nchi ikiwemo raia. Mfano, kundi la waasi likiibuka na kuanza kushambulia raia, Serikali haiwezi kukaa kimya, italazimika kuingia vitani ili kuokoa maisha ya watu na nchi. Kwasababu hiyo basi, sheria za kimataifa zinataka pakiwa na ulazima wa kupiganwa vita, lazima vita hivyo vifuate sheria za kimataifa zinazowaelekeza wapiganaji nini kinaruhusiwa kufanyika na nini hakiruhusiwi kufanyika ndani ya uwanja wa vita. Mfano mwingine wa vita vya muhimu ni; vita vya ukombozi toka kwa wakoloni, vita dhidi ya uasi katika nchi mbalimbali Afrika, vita dhidi ya uchokozi wa nchi tuliyoifanya dhidi ya ***Idi Amini Dadaa*** wa Uganda n.k.

Sheria za kimataifa zinatambua aina za vita kama za kimataifa, au vile vinavyotokea ndani ya taifa moja (*vita vya ndani ya nchi mfn; DR Congo, Jamhuri ya Africa ya Kati, Somalia na vita mbalimbali vilivyotokea Rwanda na Burundi miaka ya tisini*). Neno vita halitakiwi kuchanganywa na bughudha zingine zenye sura hiyo, kipimo kufikia uwepo wa vita huangaliwa kiwango cha uzito wa mapigano, upinzani na majibizano na mfumo wa kiutawala na kiuongozi ndani ya pande zinazopigana.[31]

Vita vya kimataifa vinaongozwa na ***Mikataba minne (IV) ya Geneva ya tarehe 12 Agosti 1949***na nyongeza yake ya ***kwanza (I) ya*** Mikataba hiyo, wakati vita vya ndani ya nchi (*hivi sio vya kimataifa*) vinaongozwa na Ibara inayotambulika kwenye kila mikataba hiyo minne ya Geneva ikitoa muongozo wa namna vita visivyo vya kimataifa vinavyotakiwa kupiganwa (***Common Article 3of the Geneva Conventions***).

Vita inatambulika kama ni ya kimataifa endapo mataifa mawili yataingia vitani au endapo vita moja itapiganwa na nchi au ndani ya nchi zaidi ya moja.

Judgement, 17 Jan. 2005, 544. See a **Blaškid, AJ** 113 – 115; Mrkšid, AJ 35; Martid, AJ 313; Blagojevid et al., TJ, 544.

[31]**Article 8 of the ICC Statute**. Na pia angalia kesi ya **Prosecutor v Tadic**, Case No. IT-94-1 (Appeals Chamber), Decision of the Defence Motion for Interlocutory Appeal on Jurisdiction, October 2, 1995, para. 70.119

Lakini vita itatambuliwa kuwa sio ya kimataifa kama itapiganwa ndani ya nchi, mfano ni kati ya Serikali ya DR Congo na waasi au kati ya kundi moja la waasi na kundi jingine ndani ya nchi hiyo hiyo moja. Umuhimu wa kutofautisha na kufahamu vyema sheria hizi unahitajika wakati wa kuandaa mashitaka dhidi ya mtuhumiwa, kila aina ya vita mashitaka yataandaliwa kwa mujibu wa sheria inayoongoza.

Katika sheria za kivita, kosa la kivita litasemekana limetendeka kama mtuhumiwa atakuwa amelitenda kama moja ya shughuli za kivita kwa eneo na mhusika mwenyewe akiwa mpiganaji wa vita husika. i.e. limefanyika katika eneo la kivita, au mhusika wa tukio ni mpiganaji wa vita inayoendelea eneo husika, au vyote kwa pamoja. Vita vinavyoendelea lazima viwe ndivyo vilivyomsukuma mkosaji kufanya kosa hilo kwa namna alivyolitenda na namna nia yake kutenda kosa hilo inavyoonyesha, kiushahidi.[32]

Jumuiya ya kimataifa imeasili sheria za kimataifa za kivita, lengo kuu likiwa ni kuwalinda watu ambao kwa wakati huo, hawajihusishi na vita na pia kuwaongoza wapiganaji kupigana vita vya kistaarabu kwa mujibu wa masharti ya kivita kama yalivyowekwa na Mikataba hiyo ya Geneva.

Kabla ya vita ya kwanza ya dunia hadi wakati wa vita vya pili, ulimwengu ulishuhudia vita nyingi zikipiganwa kishenzi (bila ustaarabu) na Mikataba ya Geneva tajwa hapo juu iliundwa ili kuzuia baadhi ya matendo yasitendeke tena katika mazingira ya vita viwe vya Kitaifa au vya Kimataifa.

Kwa mujibu wa ***Ibara ya 8(2) ya Sheria ya Mahakama ya ICC***, vitendo vifuatavyo vimeorodheshwa ndani ya Mikataba ya Geneva ili kulinda watu au vitu wakati wa mapigano ya vita, na yeyote anayekiuka vitendo hivi atahesabika ametenda kosa la kivita: -

8(2)(a): -

(i) Mauaji ya makusudi (yaliyokatazwa ndani ya Mikataba ya Geneva)

(ii) Mateso au Vitendo visivyo vya ubinadamu, ikiwa ni pamoja na kufanyia watu walioko mazingira ya kivita utafiti wa kibaolojia.

(iii) Kusababisha kwa makusudi mateso makuu au majeraha mazito ya mwili au afya (kinyume na sheria za kivita).

(iv) Uharibifu mkubwa na unyang'anyi wa mali ambazo hazijahalalishwa kivita kiumuhimu wa kivita na vinavyochukuliwa kinyume na sheria au bila kujali kunakosababisha madhara.

[32]Angalia kesi ya **Prosecutor v. Kordic and Cerkez**, Case No. IT-95-14/2 (Trial Chamber), February 26, 2001 para. 32. pia angalia **Article 8(2)(a), (c) &(e) Article 8(2)(c) vya ICC statute.**

(v) Kumlazimisha mateka wa vita au watu wanaolindwa na sheria za kivita, kuhudumu ndani ya kambi ya adui.

(vi) Kwa makusudi, kukiuka haki ya mateka wa vita au mtu yeyote anayelindwa na sheria za kivita, haki ya kusikilizwa mbele ya Mahakama inayotoa haki.

(vii) Kufukuza nje ya nchi, kuhamisha au kuweka kizuizini kinyume na sheria.

(viii) Kuteka nyara.

Ibara ya 8(2)(b) ya Sheria ya Mahakama ya ICC inaeleza kuwa, ukiukaji mwingine mkubwa wa sheria na mila zinazotumika katika vita za kimataifa ndani ya sheria za Kimataifa, unaohusisha vitendo vifuatavyo:

(i) Kwa makusudi, kulekeza mashambulizi kwenye makazi ya raia au dhidi ya raia wasiojihusisha na vita husika.

(ii) Kwa makusudi, kuelekeza mashambulizi dhidi ya mali za raia zisizo za kivita.

(iii) Kuelekeza mashambulizi dhidi ya wafanyakazi, vitendea kazi, mali, kamambi au magari yanayojihusisha na kusaidia waathirika wa vita au walinzi wa Amani kulingana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa, maadamu watu hao au vitu hivyo vinayo haki kisheria kulindwa ndani ya uwanja wa vita.

(iv) Kuelekeza mashambulizi, wakati ukielewa kuwa shambulizi hilo laweza kusababisha raia kupoteza maisha au kuharibu mali za raia au madhara ya kuenea, madhara ya muda mrefu au madhara makubwa kwenye mazingira asili, ambayo ni mazito kupita kiasi ukilinganisha na umuhimu wa kivita uliopelekea shambulizi hilo kufanyika eneo hilo.

(v) Kushambulia, au kupiga mabomu, kwa namna yeyote ila, miji, vijiji, makazi au majengo ambayo hayana umuhimu au ya kulengwa kijeshi na ambayo hayana utetezi.

(vi) Kuua au kujeruhi mpiganaji ambaye baada ya kuweka silaha chini au kuwa katika hali ya bila utetezi (hana silana n.k), kama amejisalimisha.

(vii) Matumizi mabaya ya bendera ya kusimamisha mapigano, ya bendera au alama za kijeshi na sare za jeshi la adui au za Umoja wa Mataifa pamoja na alama mahsusi za Mikataba ya Geneva, hata kusababisha kifo au majeraha mazito.

(viii) Nchi vamizi kuhamisha, moja kwa moja au kwa mlango wa nyuma, raia wake toka nchini kwao kwenda nchi iliyovamiwa, au kuhamishia nje ya

nchi watu wote au baadhi yao toka nchi iliyovamiwa kwenda ndani au nje ya nchi yao.

(ix) Kwa makusudi kuelekeza mashamulizi kwenye majengo ya ibada, elimu, Sanaa, sayansi au yanayotumika kutolea misaada, majengo ya kihistoria, hospitali na maeneo ambayo wagonjwa au majeruhu hukusanywa, maadamu sio walengwa wa kivita.

(x) Kukata viungo vya wenye madaraka katika kambi ya adui, au kuwafanyia utafiti wa dawa au kisayansi wa aina yeyote ambao haulalalishwi na matibabu ya dawa, meno au matibabu ya hospitali kwa mhusika na ambao haukufanyika kwa maslahi yake, na unaosababisha kifo au hatari kiafya kwa mhusika.

(xi) Kuua au kujeruhi kiusaliti watu toka nchi taifa adui au jeshi.

(xii) Kutangaza kuwa hakutakuwa na msamaha kwa maadui watakao jisalimisha.

(xiii) Kuharibu au kuchukua mali za adui, labda kama utaharibu au kuchukua mali hizo kwa malengo muhimu ya kivita.

(xiv) Kutangaza kufuta, kusimamisha au kutoruhusu mkondo wa sheria kutoa haki kwa raia toka nchi ya adui.

(xv) Kulazimisha raia wa nchi adui kufanya vita dhidi ya nchi yao wenyewe, hata kama walijishughulisha na vitendo vya kivita kabla vita haijaanza (lakini kwa wakati huo ni raia wa kawaida).

(xvi) Kupora mali maeneo yaliyotekwa wakati wa vita

(xvii) Kutumia sumu au silaha za sumu katika uwanja wa vita.

(xviii) Kutumia silaha zinazodhuru mfumo wa upumuaji, silaha za sumu au gesi na majimaji ya aina hiyo au nyezo za aina hiyo.

(xix) Kutumia risasi zinazotawanyika kirahisi mwilini mwa binadamu, kama vile risasi zenye kasha gumu lisilofunika kabisa kiini au iliyochanwa au kutobolewa.

(xx) Kutumia silaha, kombora na kitu au njia ya kivita inayosababisha majeraha au mateso yasiyo ya msingi ambayo ni ya kibaguzi kinyume na sheria za kimataifa za kivita, labda ziwe zinaruhusiwa na Sheria hii (ya ICC), kwa mabadiliko ya sheria kwa muhibu wa ibara za 121 na 123.

(xxi) Kufanya matukio ya kutisha dhidi ya utu, yanayodhalilisha na kushusha hadhi.

(xxii) Kufanya ubakaji, utumwa wa ngono, ukahaba wa lazima, mimba za lazima kama zilivyotafsiriwa na Ibara ya 7(2)(f), kuondoa kizazi kwa nguvu au matendo mengine yeyote ya unyanyasaji kijinsia yanayokiuka kwa hali ya juu Mikataba ya Geneva.

(xxiii) Kutumia uwepo wa raia au watu wengine wanaolindwa na sheria za vita ili kufanya maeneo hayo yasiwe ya kushambulia katika uwanja wa vita

(xxiv) Kwa makusudi kushambulia majengo, vitu, nyenzo za dawa na usafiri au watu wanaotumia alama zinazotambulikana Mikataba ya Geneva kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

(xxv) Kwa makusudi kutumia njaa kwa raia kama njia ya kivita kwa kuzuia vitu muhimu kwa ustawi wao, ikijumuisha kuzuia misaada kuingia kama ilivyoelewa na Mikataba ya Geneva.

(xxvi) Kuorodhesha watoto chini ya miaka kumi na tano (15) kwenye jeshi la nchi au kuwatumia watoto hao kama wanajeshi vitani.

Kwa vita ambavyo sio vya kimataifa, yaani vile vinavyopiganwa ndani ya nchi (mfano, vita vya wenyewe kwa wenyewe ndani ya nchi, vita kati ya Serikali ya nchi dhidi ya waasi, vita kati ya kikundi kimoja cha waasi dhidi ya kikundi kingine, vita vya kidini kati ya kikundi kimoja dhidi ya kingine n.k), ukiukwaji wa hali ya juu wa ibara ya tatu inayotokea kwenye mikataba yote ya Geneva (**common article 3**), yafuatayo ni matendo yanayokatazwa kufanywa dhidi ya raia au watu wasiojihusisha na vita, ikijumuisha wapiganaji waliojisalimisha na wasiopigana kutokana na ugonjwa, majeraha, kuwekwa kizuizini n.k.

Ibara ya 8(2)(c); -aya ya (d) ya ibara hii pia, inafafanua utofauti kati ya vita vya ndani na fujo za kawaida na maandamano yanayoweza kutokea nchini. Aya hii inasema **ibara ya 8(2)(c)** inasimamia vita vya ndani ya nchi na haijumuishi usumbufu wa kawaida na mvutano kama vile maandamano, fujo maeneo maalumu na ya mara kwa mara yenye uchaguzi na vitendo vinavyofanana na hivyo. Matendo hayo ni: -

(i) Matumizi ya nguvu kwa maisha na watu, yaani mauaji ya aina zote, kukata viungo, ukatili na mateso.

(ii) Vitendo dhidi ya utu, kama vile unyanyasaji na matendo yanayoshusha utu.

(iii) Kuchukua mateka.

(iv) Kutoa adhabu na mauaji/ kunyonga bila hukumu ya mahakama iliyopitia mfumo wote wa kisheria unaotambulika na kukubalika.

Ibara ya 8(2)(e) pia inatambua ukiukiwaji mwingine wa sheria na mila zinazotumika katika vita visivyo vya kimataifa/vita vya ndani katika mfumo uliojiimarisha kimataifa, ambayo ni: -

(i) Kwa makusudi, kushambulia makazi ya raia au watu wasiojihusisha na mapigano.

(ii) Kwa makusudi kuelekeza mashambulizi dhidi ya majengo, vitu, mahali pa kutolea dawa na usafirishaji na wafanyakazi wanaotumia alama maalumu za Mikataba ya Geneva kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

(iii) Kwa makusudi kuelekeza mashambulizi kwa wafanyakazi, vituo vyao, vitu vyao au makambi au magari yao yanayotumika katika msaada wa kibinadamu au kutunza Amani kwa mujibu wa Sheria ya Umoja wa Mataifa, maadamu vitu hivyo vinalindwa na sheria za kimataifa katika uwanja wa vita.

(iv) Kwa makusudi, kushambulia majengo ya ibada, elimu, Sanaa, sayansi au majengo ya kutolea misaada, majengo ya kihistoria na maeneo wanakohifadhiwa wagonjwa, majeruhi, maadamu wasiwe walengwa wa vita.

(v) Kupora mali miji au maeneo yaliyotekwa, hata kama yametekwa kinguvu

(vi) Vitendo vya ubakaji, mateka wa ngono, ukahaba wa lazima, mimba za lazima kama ilivyofafanuliwa na kifungu cha 7(2)(f), kusababisha utasa wa lazima na matendo mengine yote ya unyanyasaji kijinsia kama yalivyokatazwa na ibara ya tatu iliyopo katika mikataba minne (4) ya Geneva.

(vii) Kuhusisha au kuwaingiza watoto chini ya miaka kumi na tano (15) katika vita au kundi au kuwatumia dhidi ya maadui.

(viii) Kuamuru kuondolewa raia kwa sababu zinazofanana na mgogoro uliopo, labda kama usalama wa raia hao eneo la vita ni wa muhimu.

(ix) Kuua au kujeruhi kiusaliti adui wa mpiganaji.

(x) Kutangaza kwamba hakuna adui atakayekubaliwa akijisalimisha.

(xi) Kukata viungo vya viongozi wa maadui, au kuwafanyia utafiti wa dawa au kisayansi wa aina yeyote ambao haulalalishwi na matibabu ya dawa, meno au matibabu ya hospitali kwa mhusika na ambao haukufanyika kwa maslahi yake, na unaosababisha kifo au hatari kiafya kwa mhusika.

(xii) Kuharibu au kuchukua mali za adui, labda uharibifu huo au uchukuaji huo iwe ni kwa maslahi ya vita.

KUMBUKA: Kwa kuhitimisha, **ibara ya 8(3)** ya **Sheria ya Mahakama ya ICC** inaeleza kwamba, masharti yaliyowekwa katika **Ibara ya 8(2) (c)** na **8(2)(e)** hayataathiri wajibu wa Serikali kuendeleza au kujenga upya misingi ya sheria na utulivu katika nchi, au kutetea umoja na ustahimilivu wa nchi

4) Kosa la Uchokozi kwa nchi (Crime of Aggression)

Hili ni kosa gumu na lililobanwa kuliko yote katika kufanikisha mashitaka ya viongozi wa nchi au makamanda wa jeshi wa nchi. Kosa hili linalenga moja kwa moja kushitaki viongozi wanaoongoza uchokozi kwa nchi nyingine, kinyume na vigezo vilivyowekwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter). Uchokozi unaoongelewa ni uchokozi wa kijeshi au vitendo vinavyoashiria vita, vilivyozuiwa na ***Mikataba ya Geneva ya tarehe 12 Agosti, 1949***, kama vikifanyika dhidi ya watu au mali zinazolindwa na Mikataba hiyo. Ibara ya **8(1) & (2) *bis*** ya Sheria ya ICC inafafanua kosa la uchokozi kama: -

> "*kupanga, kuandaa, kuanzisha au kufanya kwa mtu aliyepo kwenye nafasi ya utawala au kuongoza nchi kisiasa au kijeshi, tendo la uchokozi ambalo kwa uzito na ukubwa linaonyesha ukiukwaji wa wazi wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.*

KUMBUKA: kosa hili linalenga zaidi viongozi wa kisiasa na viongozi wa kijeshi kwa maana ya mtu ambaye yupo katika nafasi ya kutawala kikamilifu na kuongoza wengine kisiasa au kijeshi kutenda jambo dhidi ya nchi nyingine. Kwa juujuu, viini vya kuthibitisha kosa Mahakamani ni kama kiongozi huyo alishiriki katika kupanga, kuandaa, kuanzisha au kutenda jambo la kichokozi dhidi ya nchi nyingine ambapo kwa muono wa wazi iwe ni kinyume na vipengele vya Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter) vinavyotawala mazingira ya aina hiyo. Matendo yafuatayo iwe imetangazwa vita ama la yanaunda kosa la uchokozi dhidi ya nchi:-[33]

(a) Kuvamia au kushambulia nchi nyingine kwa kutumia jeshi au kutokana na kuvamia nchi vamizi inaweka kambi ya kijeshi kwenye nchi nyingine hata kama ni kwa muda mfupi, au kujimilikisha kwa nguvu kipande chochote cha nchi nyingine.

(b) Kwa kutumia jeshi, kupiga mabomu au kutumia silaha yeyote ile dhidi ya nchi nyingine.

(c) Kwa kutumia Jeshi, kufunga njia za Bandari au ufuo wa pwani wa nchi nyingine (kuzuia mizigo kuingia kwa kutumia bahari au njia nyinginezo za pwani).

[33] This is in accordance with United Nations General Assembly resolution 3314 (XXIX) of 14 December 1974

(d) Kwa kutumia jeshi, kushambulia ardhi, jeshi la bahari au la anga au nyenzo za kivita za bahari au anga vya nchi nyingine.

(e) Matumizi ya jeshi yanayokiuka masharti ya makubaliano, kwa jeshi la nchi fulani lililokubaliana na nchi nyingine kuingia na kuweka kambi kwake, au pale jeshi lililopokelewa kuweka kambi kujiongezea muda wa kuendelea kuwepo kwenye nchi iliyolipokea jeshi hilo hata baada ya muda uliowekwa kwenye makubaliano kwisha. **Mfano**: Mkataba/Makubaliano yanaingiwa kati ya nchi fulani kwamba nchi nyingine ya kigeni iweke kambi ya kijeshi nchini mwake, lakini baada ya kambi ya jeshi ya nchi hiyo ya kigeni kuwepo kwenye hii nchi pokezi, jeshi katika kambi hiyo ya kijeshi ikavunja masharti yaliyowekwa kwenye mkataba uliowapa hifadhi au hata baada ya muda wa kambi yao kuwepo kwenye nchi pokezi kwisha, jeshi hilo la nchi ya kigeni likang'ang'ania kwa kutumia nguvu kuendelea kuwepo kwenye nchi pokezi. Huo utakuwa uchokozi.

(f) Kitendo cha kuruhusu ardhi ya nchi yako iliyopakana na nchi nyingine, kutumika na nchi nyingine kuvamia nchi nyingine/ya tatu. **Mfano:** nchi "**A**" ana nia ovu dhidi ya nchi "C" na katikati yao wote wamepakana na nchi "**B**"; na kwasababu nchi "**A**" anahitaji kuvamia nchi "**C**" iliyopakana moja kw amoja na "B", nchi "B" inaruhusu ardhi yake itumike na nchi "**A**" kushambulia au kuvamia nchi "**C**".

(g) Nchi kutuma au kuwakilishwa kwa kutuma vikosi vyenye silaha, makundi yenye silaha, wanamgambo au mamesenari wenye nguvu ya kijeshi dhidi ya nchi nyingine, kwa nguvu ya kijeshi inayotafsiriwa na vitendo vilivyoorodheshwa hapo juu au vinavyojihusisha hivyo kwa namna fulani.

NB: Kosa la uchokozi ni gumu na linapingwa na nchi nyingi wanachama wa Mkataba wa Roma, na tangu ***Julai 17, 2018*** limewekwa katika mazingira ya uhuru wa nchi wanachama kulikubali, kulikataa au hata baada ya kulikubali hapo mbeleni kuja kujiondoa kwalo.

Nchi isiyo mwanachama wa ICC, au mwanachama ambaye hajasaini kulikubali kosa hili au aliyesaini na baadaye kujiondoa, raia wake hawatashitakiwa kwa kosa hili au hata raia wa nchi nyingine akitendea kosa kwenye nchi isiyohusika na kosa hili hatashitakiwa, labda maombi yawe yamepelekwa ICC kwa azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Cha ajabu ni kwamba, mataifa yote makubwa kama vile, **Marekani, Urusi, Uchina, Muungano wa Kifalme (UK)** n.k si wanachama wa ICC. Pia hizo ndizo zenye mamlaka ya VETO (USA, Urusi, China, UK & Ufaransa) ni ngumu watu wake kushitakiwa. Hii maana yake, mataifa makubwa ambayo mara nyingi ndio huvamia nchi nyingine, wakuu wao wa nchi au Makamanda wa jeshi, hawatashitakika kwasababu sio wanachama au hawajasaini kukubaliana na kosa hilo kwa mujibu wa ibara ya **15(5)** ***bis***. Tunasema hivyo

kwasababu likaapo Baraza la Usalama kuazimia kama tuhuma ipelekwe ICC au la, nchi hizo za VETO lazima zinakuwepo na zinayo nafasi kupinga Azimio la Baraza dhidi ya raia wao katika kosa hili la uchokozi kwa nchi.

Ibara ya **15(4)(5)** ***bis***, inaeleza kwamba: -

> ***(4)*** *Mahakama itakuwa na mamlaka kushitaki kosa la uchokozi kwa nchi uliofanywa na nchi mwanachama, labda nchi hiyo iwe imetangaza kabla kutokukubaliana na mashitaka ya kosa la uchokozi kwa kupeleka maelezo hayo kwa Msajili wa Mahakama. Kujiondoa kwenye tangazo hili kwaweza kufanyika na kutazingatiwa na nchi mwanachama katika kipindi cha miaka mitatu (3).*
>
> ***(5)*** *Kwa nchi ambayo si mwanachama wa Mahakama ya ICC, Mahakama haitakuwa na mamlaka dhidi yake kwa kosa la uchokozi kwa nchi uliofanywa na raia wake au uliofanywa kwenye nchi yake.*

NAMNA CHUKI INAVYOZALISHWA NA KUENEA

Matendo ya chuki, uhasama na ugomvi ndiyo yamekuwa msingi wa makosa yote yanayoendeshwa na ICC. Kwa kawaida, chuki inazaliwa kwa inasababishwa na vitu vingi; inaweza kusababishwa na ***viongozi wa dini kuhubiri chuki*** dhidi ya dini nyingine na kwasababu wananchi wanawaamini sana kiroho wakabadilishwa mioyo, ***viongozi wa kisiasa kuhubiri chuki*** dhidi ya Serikali au kundi jingine la kisiasa kutokana na kugombania madaraka, ukabila kama zilivyo nchi kadhaa majirani, ***vinyongo mbalimbali vinavyodumu muda mrefu mioyoni mwa watu*** kwasababu mbalimbali na vinavyosababishwa na chanzo kimoja kwa wote, ***Serikali kuzembea kuwajibisha vyombo vya habari kama magazeti***, radio, television na kwa enzi hizi ni mitandao ya kijamii n.k.

PAMOJA NA YOTE, kuwepo na chanzo chochote cha chuki hakuhalalishi raia yeyote kufanya makosa kwasababu jinai siku zote hailipi na wakosaji wote hujuta baadaye. Wakosaji wote ambao walishawahi kushitakiwa ICTY, ICTR, Special Court for Sierra Leon, Special Tribunal for Lebanon, Cambodia na sasa ICC, wangelipewa nafasi ya kurudi nyuma wasingefanya yale waliyoyafanya yakawapelekea kushitakiwa. Hii ni kwasababu yeyote anayefanya makosa ya jinai za kimataifa haangaliwi tu nan chi yake bali jumuia ya kimataifa.

Tujifunze kwa yaliyotokea Rwanda kabla na mwaka 1994

Ijulikane kuwa, kwa upande wa **Kosa la Kimbari**, kama miongoni mwa Makosa manne yanayoshitakika Mahakama ya ICC, haliji ghafla, huja taratibu likirutubishwa na **chuki inayogawanya watu kwa minajili ya taifa, kabila, rangi au dini** hadi kufikia wakati watu wa kundi fulani kuwachukia na kuwaondolea ubinadamu watu wa kundi jinguine.

Mwaka 1994 nchini Rwanda, ndani ya siku 100 tu, Watutsi kati ya 800,000 hadi 1,000,000 waliteketezwa. Hii ni idadi kubwa sana ya watu na ilisababishwa na chuki za muda mrefu dhidi ya kabila lingine kabla ya hapo. Katika hatua hii, mtu aliyelishwa sumu ya chuki, uadui na mgawanyo huwa kipofu kabisa wa akili na anaweza kuendeshwa hata kwa kupulizwa na upepo tu kufanya lolote atakaloambiwa na kiongozi wake au kufuata mkumbo makundi ya kihalifu.

Mfano wake ni kwamba, kama sumu ya chuki ilikuwa ni ya kidini, mdini huyo anaweza kuwa kipofu kabisa wa akili dhidi ya watu wa dini nyingine na kufanya jambo lolote la kikatili bila kufikiria matokeo, pamoja na kwamba siku akikamatwa na vyombo vya dola ya nchi au dunia, huwa anajuta na kutamani laiti asingekuwa ametenda kosa hilo. Cha msingi ni nchi husika kushughulikia wasambaza chuki za kidini, kitaifa, kikabila na rangi wote kwa mujibu wa sheria mapema kabla hazijazaa matatizo katika jamii.

Ni jambo la kweli kuwa ulikuwepo uhasama kati ya jeshi la Serikali na waasi wa RPF kipindi hicho Rwanda kabla na mwaka 1994, lakini waliouawa katika mauaji ya kimbari ni raia ambao hata hawakuwa na silaha na hawakuwa msituni wakipigana; wanawake, watoto, wazee, walemavu ambao hata hawakuwa na uwezo wa kujilinda walikaa wakisubiri kuuawa kwasababu ya chuki iliyosambazwa na kudumu kwa muda mrefu tena ikibarikiwa na viongozi wakubwa tu wa Serikali ya kipindi hicho.

Cha muhimu kuelewa ni kwamba, yatokeapo matatizo kwenye nchi, nchi hiyo na watu wake ndio watakaoathirika; nchi nyingine zinaweza zisitoe msaada wowote na hata kujiweka pembeni. **Mfano**, wakati wa Mauaji ya Kimbari Rwanda 1994, mataifa ya magaribi ambayo ndiyo yanayojinadi kuwa yamefikia ustaarabu wa juu kabisa na yanayolinda haki za binadamu **(ikiwemo haki ya kuishi**), yalikuwa mstari wa mbele kutuma ndege kuondoa raia wao Rwanda na kuwaacha raia wa Kinyarwanda mikononi mwa wauaji. Wauaji nao wakiwa tayari na silaha walikaa kusubiri raia wa Magharibi waondoke ili waanze kazi ya kuua.

Wanadiplomasia wengi walioondolewa Rwanda kipindi hicho wanaeleza kushuhudia ***Intalahamwe*** na ***Impuzamugambi*** wakiwa na mapanga mkononi wakisubiri wao waondoke ili waanze kazi ya kuua. Nchi hizo pia zenye uwezo mkubwa kijeshi hazikutuma ndege na wanajeshi kusitisha mauaji bali ndege zao za kijeshi na wanajeshi waliotumwa kwa ustadi mkubwa kabisa walienda Rwanda kuokoa/kuhamisha raia wao tu na si kuwaondoa wanyarwanda waliokuwa katika hatari ya kuuawa. Kulikuwa na nafasi ya kuokoa maisha ya wengi kama mataifa yote yangejali, si kitu cha kawaida watu zaidi ya laki nane kuuawa ndani ya siku 100 tu.

Unaweza kupata picha mtoto wa Kinyarwanda alivyokuwa anafikiri moyoni mwake, anapoona magari na ndege yanawachukua raia wa kigeni tu ikijumuisha pia mifugo kama mbwa na paka n.k kuwapandisha kwenye ndege

zilizotumwa, na kuwaacha wao mikononi mwa watu wanaosubiri ndege na wageni hao waondoke ili waanze kazi ya kuua.

Chuki na Uadui Rwanda kabla na wakati wa Mauaji ya Kimbari

Kutolea mifano nchi nyingine kama Rwanda ambako tayari umoja na maridhiano vilishafanyika, na nchi inapiga hatua kimaendeleo, hatuandiki ili kukumbusha vidonda vilivyokwishapona na watu ambao tayari wamesameheana. Kwasababu ukweli upo wazi kwamba makosa ya kimbari yalitokea na hata kwa uwepo wa makumbusho ya kimbari "***genocide memorial***" jijini Kigali, ni muhimu jamii nyingine duniani kujifunza chanzo au vichocheo vya yaliyotokea mwaka 1994 ili kuzuia yasitokee tena katika nchi nyingine yeyote milele. Yafuatayo ni baadhi ya yaliyotokea 1994.

1. Kuwafananisha Watutsi na wadudu

Maelezo haya hayataenda kuanzia miaka ya 1959 wakati wa mapinduzi ya Kihutu. Nikianzia mapema kabla na wakati wa mauaji ya kibari Rwanda 1994, ***wanasiasa, waandishi wa habari, wanamuziki*** pamoja na ***watu waliokuwa na ushawishi*** kwa raia walihubiri sana chuki dhini ya Watutsi jambo lililosababisha mgawanyiko mkubwa sana wa kikabila nchini Rwanda.

Mbinu moja wapo iliyotumika ni kuwafananisha Watutsi na wadudu; Waliwaita mende (***cockroach-Inyenzi***), na wasambaza chuki walifanikiwa kuingiza kwenye vichwa vya watu wa kabila la Wahutu hoja kwamba Watutsi ni wageni wala si raia wa Rwanda, wametoka huko Ethiopia. Kwa njia hii, chuki kati ya Wahutu na Watutsi ilizidi sana kiasi kwamba Wahutu waliamini kuwa Watutsi hawastahili kuishi au kutawala Rwanda.

Mfano: mwaka 1992 kiongozi mmojawapo wa Rwanda kipindi hicho alisikika akiongea kwenye mkutano kuwa watusi sio raia wa Rwanda, ni wageni, na wangetafutiwa njia ya mkato kuwarudisha kwao, njia ambayo ingekuwa kuwaua na kuwatupa kwenye mto Nyabarongo wachukuliwe na maji hadi Ethiopia. Kwenye mkutano huo alisema; -

> *"They (the Tutsi)belong in Ethiopia and we are going to find a shortcut to get them there by throwing them into the Nyabarongo River….Wipe them all out"*,[34]
>
> *"wao (watusi) ni Waethiopia na tunaenda kutafuta njia ya mkato kwao kufika kule kwa kuwatupia mwenye mto Nyabarongo…futa wote"*

Ikitokea mtu wa nchi nyingine ya leo kuwabagua kwa kuwafananisha watu wa kundi fulani na wadudu au wanyama, sio jambo la kudharau au kulichekea. Ni muhimu kuhakikisha wasambaza chuki wote wanashughulikiwa kisheria kabla hawajaleta madhara kwa raia.

[34] Ukisoma kitabu cha " Prunier at 172" utaelewa ninachoongelea.

2. Propaganda za vitisho kwa wananchi.

Zaidi ya kuwaita Watutsi "**mende**", neno lingine lililohamasisha chuki ni kuwaita Watutsi watu wa "**ukoo wa kifalme**" kutokana na historia kwamba Wafalme wa Kitutsi waliwatawala kwa muda mrefu Wahutu katika eneo hilo na Wahutu walikuwa hawapendi kusikia kitu hicho. Inasemekana kwa miongo kadhaa na karne, Watutsi walitawala Rwanda na hata wakati wa ukoloni wao ndio walipewa kipaumbele cha kusoma na nafasi katika utawala wa kikoloni.

Kwahiyo kwasababu Mhutu hapendi kutawaliwa na Mtutsi, ukiwaita Watutsi "**ukoo wa Kifalme**" ilitegemewa kuleta hasira, kuchukiza na kuwaunganisha Wahutu dhidi ya Watutsi. Ikizingatia kwamba nchini Rwanda wakati huo utawala ulikuwa wa Rais ambaye ni Mhutu, na Waasi wa Kabila la Kitusi wakishambulia kutokea Uganda, wasambaza chuki walisambaza vitisho kwamba "**hao watu wa kifalme**" wanakuja kutoka jeshi la waasi kututawala tena kama ilivyokuwa kabla. walichagua aina ya maneno na mazingira yatakayorahisisha chuki isambae haraka na kwa matokeo makubwa. Kama nilivyokwisha kueleza kwamba, neno "**watu wa ukoo wa kifalme**" yalikuwa maneno yanayochukiza sana na wasambaza chuki walilifahamu hilo na walihakikisha wanachagua maneno sahihi yanayoweza kuchukiza.[35]

Nchi nyingine, zijifunze kutokana na misamiati na nahau zinazotumika katika lugha husika yanaweza kuwepo maneno ambayo sio ya kichochezi moja kwa moja lakini yakitamkwa jamii husika inakuwa imehamasishwa kwa mlango wa nyuma na kuleta madhara katika jamii.

3. Wachora vikatuni

Wachora vikatuni nao wana mchango mkubwa kusambaza au kuzuia chuki miongoni mwa jamii. Mfano, mwaka 1991 gazeti moja Rwanda lililoitwa ***Echo des 1000 collines***lilichora kikatuni chenye maneno: -

> "*Kimbia, Mtutsi watawateketeza Wahutu" Flee! A Tutsi will exterminate the Hutus.*"

Sote tunajua lugha za vikatuni ni kitu kidogo lakini kina maudhui makubwa. Hii ilikoleza chuki na kuunganisha Wahutu katika kuwashambulia raia wa kabila la Watutsi waliokuwa Rwanda ambao hawakushiriki vita, na wala hawakuhusika kabisa na ugomvi wa kimadaraka wa wanasiasa wa wakati huo.

4. Watu mashuhuri na viongozi kutoa matamshi ya chuki na vitisho kwa wananchi

Mtu mashuhuri/maarufu au kiongozi ni rahisi sana kusikilizwa au kuaminiwa na jamii. Wakati wa mauaji ya Kimbari Rwanda 1994, Mwanasiasa

[35]ALISON DES FORGES, (1999) "LEAVE NONE TO TELL THE STORY": GENOCIDE IN RWANDA at 72.

mmoja aitwaye "**MUGESERA**" katika kesi iliyoendesha Canada, ushahidi dhidi yake ulionyesha alisikika kwenye hadhara akiwaita Watutsi Mende wenye mpango wa kuwateketeza Wahutu nchini Rwanda, na alilenga kuwatisha na kuwaunganisha Wahutu ili kwa pamoja wawateketeze Watutsi. nikinukuu: -

> *"hawa watu wanaoitwa **mende** wanakuja kutushambulia…nawaambieni, na wala siwadanganyi, ni kweli…wanataka kututeketeza sisi, wanataka kututeketeza wala hawana lengo jingine. Je? Tunasubiri tu hadi waje watuteketeze?"* [36]

Ikizingatiwa wakati huo watu walioitwa mende hawakuwa wale tu wa msituni, bali Watutsi wote hata raia walioko mtaani, watoto, wazee n.k,

Katika kesi hiyo, mtu mmoja aliyeitwa **Alfred Kiruhara**, aliyekuwa mkulima wa kawaida kabisa kipindi cha mauaji ya kimbari Rwanda, alieleza kuwa,

> *"sikuamini kama Watutsi wanakuja kutuangamiza, lakini baada ya radio ya serikali kuendelea kulitangaza hilo kwamba walikuwa wanakuja kuchukua ardhi yetu, kuua Wahutu, ikarudiarudia mara nyingi, nilianza kuogopa."*[37]

Mnyarwanda mwingine aliyekuwa kijana mdogo kipindi hicho, alikiri kuua kwa mkono wake yeye mwenyewe wanakijiji kumi na tano (15) alieleza kuwa:

> *"Serikali ilituambia kuwa RPF ni Watutsi na kama wakishinda vita, Wahutu wote tutauawa"*

Hii ina maana kwamba, raia waligawanywa na kulishwa sumu ya chuki kiasi kwamba mhutu aliamini mtusi hata yule wa mtaani asiye na silaha ana nia ya kuwaua wahutu, hivyo raia wasio Watutsi wangeshiriki kuwateketeza Watutsi kabla Watutsi hawajawateketeza wao kama walivyoambiwa na viongozi.

5. Kutumia misamiati, nahau au mafumbo

Kuna baadhi ya maneno katika jamii yanavyotamkwa ni tofauti na yalivyowekwa kueleweka kwenye jamii husika. Mfano, wakati wa mauaji ya kimbari Rwanda 1994, baadhi ya nahau/misamiati katika macho ya kawaida inaweza kuonekana ya kawaida lakini iliwekwa ili kuleta athari kubwa sana wakati wa mauaji. Mfano: -

"Nendeni kazini" *ikimaanisha**, nendeni kuua Watutsi".***

Hivyo raia wa kawaida akiambiwa "**umeshaenda kazini**" au "**nendeni kazini**" alielewa kinachomaanisha kwamba anaambiwa kwa mlango wa nyuma

---

[36]Mugesera v. Canada (Minister of Citizenship and Immigration), [2005] S.C.C. 40, 69, app. III 18.

[37]Christine L. Kellow & H. Leslie Steeves, The Role of Radio in the Rwandan Genocide, J. COMM., Summer 1998, at 107,
123 (citing Tharcisse Gatwa, Ethnic Conflict and the Media: The Case of Rwanda, 42 MEDIA DEV. 3, at 18–20 (1995)).

kwamba aende kuua Watutsi, kwani huo ulitumika kama msamiati wa mafumbo. Katika mashitaka Mahakamani kila neno huchukuliwa vile lilivyoeleweka kwenye jamii, hivyo hata mafumbo kama yalimaanisha kitu kibaya mkosaji hawezi kusalimika.

Pia neno **Inyenzi (mende)** ambalo mwanzoni lilimaanisha Watutsi wanaopigana msituni, baada ya kusambaza sana chuki lillikuja kujumuisha pia raia wa kawaida kabisa wa Kitutsi ambao walikuwa wanaishi palepale Rwanda ambao hawakuwa na silaha wala hawakuwa msituni kupigana na jeshi la Serikali. Wote walijumuishwa kama mende na kama wahamiaji. [38]

Mwanasiasa *Jean-Paul Akayesu*

Huyu alikuwa ni *bourgmestre au Meya wa mji wa* ***TABA***kule Rwanda. Ilisemekana kwamba, mapema asubuhi ya tarehe **19/04/1994**, Akayesu alisimama katikati ya raia 100 karibu na mwili wa mwanamgambo wa kihutu, alihutubia umati huo akiwataka washirikiane kwa pamoja kupambana na "***adui wetu sote***" aliowaita wahitimishi wa *Ikontanyi* au wa waasi wa kitusi (accomplice)[39], akimaanisha raia wa kawaida kabisa wa Kitutsi wanaoishi Rwanda [40]. Matamshi hayo yalikuwa ni ya chuki, hata hivyo, ili kuunda kosa inatakiwa mtamkaji awe alikuwa na nia kuhamasisha wasikilizaji kutenda kosa husika, jumuiya ya kimataifa imekuwa ngumu kuamini kila matamshi yasiyo na ushahidi wa nia ovu ya kuhamasisha kwa kuamini wakati mwingine mtamkaji kama hatavuka mstari anaweza kuwa anatumia haki yake ya kujieleza. *Akayesu* kwa sasa anatumikia kifungo jela nchini Mali.

Tuhuma mojawapo iliyolalamikiwa na upande wa mashitaka ilikuwa kwamba, watu wale aliowahutubia walielewa kuwa anawataka wawauwe watu wa kabila la watusi ambao yeye akiwa na akili timamu alifanya uchaguzi wa aina ya maneno ya kutumia ***"adui wetu sote" akimaanisha wahitimishi wa Ikontanyi au wahitimishi wa RPF***. Baada ya hotuba hiyo, mamia ya Watutsi raia wa kawaida kabisa mtaani waliuawa kwenye makazi yao huko TABA.

Hapa tunajifunza namna kauli za viongozi au watu wenye ushawishi zinavyoweza kusababisha madhara katika jamii kama hazikutolewa kwa uchaguzi wa aina ya maneno ya kutumia na bila hekima, vilevile tunajifunza namna mtu anavyoweza kuwajibika kwa chochote alichokifanya kama kikileta madhara; kama haujawajibishwa leo ipo siku mbeleni utakuja kuwajibishwa

---

[38]Jean-Marie Vianney Higiro, Rwandan Private Print Media on the Eve of the Genocide, in THE MEDIA AND THE RWANDA
GENOCIDE 73, 84 (Allan Thompson ed., 2007); Prosecutor v. Ruggiu, Case No. ICTR 97-32-I, Judgment and Sentence, 44 (June 1, 2000) (Georges Ruggiu, a Belgian broadcaster who pled guilty to committing incitement to genocide in Rwanda, admitted that by 1994, inyenzi had come to signify "Tutsi" and "person to be killed").

[39]Prosecutor v. Akayesu, Case No. ICTR 96-4-T, Judgment (Sept. 2, 1998).

[40] The word accomplices means "someone who helps somebody to commit a crime or misdeed", Encarta Dictionary 2009 version.

tu kwasababu jinai haifi na huwa hailipi. Cha muhimu ni kuwa makini katika kila unachokifanya katika jamii kisilete madhara.

Waziri Mkuu "Jean Kabanda"

Huyu alikuja kukiri kosa na kufungwa kifungo cha maisha. **Jean Kambanda** alikuwa ni Waziri mkuu wakati wa siku 100 za mauaji ya Kimbari Rwanda aliyetumia vibaya umaarufu wake wa kisiasa, akasambaza chuki zilizochangia pakubwa sana mauaji ya kimbari. Akiwa kiongozi mkubwa hivyo, alitumia ***Radio RTLM*** kuhamasisha mauaji ya kimbari ndhidi ya Watutsi. Waziri huyu alisema radioni kwamba, "RTLM ilikuwa silaha mahiri sana katika mapambano na maadui"[41]. Mbele ya Mahakama ya ICTR alikiri Makosa kwamba ***alitoa hotuba zenye kuhamasisha wananchi kuwashambulia Watusi na Wahutu wenye msimamo wa kati***. Kwa kinywa chake alikiri kuwa alisema redioni:-

> **"*mnakataa kujitolea damu yenu kwa ajili ya nchi yenu na mbwa wanainywa bure*"** *you refuse to give your blood to your country and the dogs drink it for nothing..."*[42]**.**

Hao mbwa alimaanisha Watutsi na watu wa kabila la Wahutu waliomsikia walielewa anamaanisha kwamba, wanakataa kuungana kuwashambulia Watutsi walioko msituni na hata raia wema wa kitutsi mtaani, hivyo Watutsi wanaowaacha watainywa damu yao. Maneno haya kutoka kwa kiongozi mkubwa wa nchi yalihamasisha mauaji ndani ya siku hizo 100.

MATUMIZI MABAYA YA VYOMBO VYA HABARI

Chombo cha habari ni nyenzo yenye nguvu na ushawishi wa haraka katika jamii zote duniani na ni rahisi kulifikia kundi kubwa la watu katika muda mfupi au kwa wakati mmoja. Kama chombo cha habari kikitumiwa vyema huleta matunda mema ya haraka kwa watu wengi, na kama vikitumiwa vibaya vyaweza kuleta madhara makubwa kwa haraka na kwa muda mfupi katika jamii. Kwa mfano, chuki au uzushi ukitolewa, waweza kuenea haraka sana na kuaminisha watu au kuunganisha watu kufanya uovu na hasa, mfano; kama ni matamshi ya watu maarufu, viongozi wa dini wanaoaminiwa, siasa wenye wafuasi wengi au kundi la watu fulani, wanamuziki n.k.

Hii imeilazimu kila jamii duniani kuweka sheria zinazodhibiti matumizi mabaya ya vyombo vya habari kutokana na kujifunza madhara yaliyotokea katika nchi kadhaa duniani. Waandishi wa habari na wanamuziki wajifunze kwa yaliyotokea Kenya, tulishuhudia waandishi wa habari wakishitakiwa na Mahakama ya ICC kutokana na fujo za uchaguzi za mwaka 2007/2008. Tutaona pia namna wanamuziki walivyoshitakiwa kwa mauaji ya Kimbari Rwanda ya mwaka 1994.

---

[41] Prosecutor v. Kambanda, Case No. ICTR 97-23-S, Judgment, 39 (Sept. 4, 1998).
[42] ibid

Kesi ya Wanahabari – ("Media case")

Katika Mahakama ya ICTR Arusha, kesi ya wanahabari "**Media case**" ilihusisha wanahabari watatu, ***Ferdinand Nahimana, Jean-Bosco Barayagwiza na Hassan Ngeze***, waliokuwa wametuhumiwa kutumia redio na gazeti kimkakati kusambaza chuki na hamasa za moja kwa moja kuwadhuru Watutsi.[43] Maelezo katika kipengele hiki yatakuwa ni machache na hatutafafanua kiundani sana lengo kuu likiwa ni kuelezea kiujumla vitendo walivyovitenda hata vikachangia mauaji ya kimbari Rwanda.

Ferdinand Nahimana
&
Jean-Bosco Barayagwiza

Ferdinand Nahimana na **Jean – Bosco Barayagwiza** walikuwa watu maarufu sana miaka ya 1993/1994 katika medali ya habari na hasa uhusika wao katika redio iliyoitwa RTLM (**Radio-Télévision Libre des Milles Collines)**. Radio hii ilianzishwa **08/04/1993** mwaka mmoja kabla ya mauaji ya kimbari na ilidumu hadi tarehe **31/07/1994**. Kabla ya kuundwa kwke, kundi la Wahutu wenye msimamo mkali, waliona redio ya Serikali (Radio Rwanda) kama ni yenye msimamo wa kati dhidi ya Watutsi,wakaamua kuunda radio mbadala RTLM iwe yenye msimamo mkali na ***Ferdinand Nahimana*** alikuwa mmojawapo wa wakurugenzi waanzilishi na pia alikuwa mmojawapo wa waanzilishi wa chama cha CDR (Coalition for the Defence of the Republic).

Inasemekana kipindi hicho redio ilikuwa nyenzo muhimu kufikisha ujumbe kwa wananchi, na kwasababu Redio Rwanda iliyomilikiwa na Serikali ilitumbuiza miziki na kuwa na mtindo wa utangazaji wa kizamani usio, usio na msimamo mkali na mhemuko kwa vijana, redio RTLM ilijikuta imepata wasikilizaji wengi sana hasa vijana kwa kutumbuiza miziki ya kisasa hasa ya Kongo miaka hiyo na ikaipiku umaarufu hata redio ya Serikali.

Kutokana na umaarufu huo na waanzilishi wa radio hiyo kuwa na uhusiano wa ndani na ***Rais Habyarimana***, Serikali iliiunga mkono ikatumiwa sana na Wahutu wenye msimamo mkali katika propaganda mbalimbali dhidi ya Watusi[44]**.** Msaada mmojawapo toka Serikalini kwa redio RTLM katika kipindi fulani ni kupitishia masafa yake kwenye mitambo ya Radio Rwanda, pamoja na viongozi wa Serikali waliohojiwa nayo kuonyesha kama ni radio ya watu yenye lengo la kuhamasisha uzalendo na utawala wa Wahutu Rwanda. Nahimana alikuwa mkurugenzi mkuu wa radio hiyo, wakati Barayagwiza alikuwa msaidizi wake, wote watatu pamoja na Hassan Ngeze wakiwa wafuasi wa chama kipya kilichojulikana kama "**CDR**".

---

[43] *The Prosecutor v. Ferdinand Nahimana, Jean-Bosco Barayagwiza, Hassan Ngeze*, Case No. ICTR-99-52-T, Appeals Judgement, 28 November 2007 ("*Nahimana et al.* Appeals Judgement"), para. 30.

[44] Kirschke, Linda (1996): Broadcasting Genocide: Censorship, Propaganda & State-Sponsored Violence in Rwanda 1990-1994, ARTICLE 19, London.:47, 70-71, Prunier supra note 8 at165, 188

Nahimana aliposhitakiwa Mahakama ya **ICTR** alieleza kuwa, lengo kuu la kuanzisha redio RTLM lilikuwa ni kama kuunda radio ya kushindana na ***Radio Muhabura*** iliyokuwa ikimilikiwa na waasi wa **RPF** kipindi hicho, jambo ambalo hata kama lingekuwa hivyo halihalalishi chuki kuhamasisha mashambulizi dhidi ya Watutsi kulikofanyika.

Radio Muhabura ilikuwa ni radio iliyoanzishwa na Waasi wa **RPF** waliokuwa Uganda kwa lengo la kujibu au kusahihisha chuki zilizokuwa zikisambazwa nchini Rwanda wakati huo dhidi ya RPF na Watusi wote hata wasio vitani [45].

Wengi wanafananisha na vyama vya siasa katika nchi mbalimbali duniani kumiliki magazeti, radio na television n.k, ni jambo jema wala sio baya kama maadili na sheria zitafuatwa. Vivyo hivyo na vyombo vya dini kumiliki magazeti, radio au television; ni jambo jema kama maadili na sheria za nchi zitafuatwa. Hata hivyo, kwa kawaida ya mwanadamu yeyote mwenye mlengo fulani, ni vigumu kwa chombo cha habari kinachomilikiwa na makundi yanayopingana kutoa habari bila chuki au kutopendelea upande mmoja; chama cha siasa sio rahisi kuongea vyema dhidi ya chama inachopigana nacho, vivyo hivyo na kwenye Imani za dini, kila mtu anavutia upande wake akitamani upande mwingine uamini chake na wakati mwingine hata kuchafua hali ya hewa. Kama wahariri hawatakuwa makini, ni rahisi kusambaza chuki dhidi ya kundi jingine la upande wa pili.

Hassan Ngeze

Kwa upande wa mshitakiwa mwingine ***Hassan Ngeze,*** huyu alikuwa mmiliki, mwanzilishi na mhariri wa gazeti maarufu la ***KANGURA*** lililosambazwa na kupendwa na wengi nchini Rwanda kipindi hicho. Kabla na wakati wa mauaji ya kimbari, gazeti hili lilisambaza chuki dhidi ya Watutsi, hofu kwa Wahutu na lilichangia pakubwa sana katika kuhamasisha na kuteketeza Watutsi nchini Rwanda [46]**.** Mojawapo ya propaganda kubwa za gazeti hili zilikuwa ni amri kumi za wahutu, mambo yaliyokuwa yameorodheshwa kuwabagua kabisa Watusi wasishirikiane na wahutu, wasioane na waonekana ni maadui wakubwa wa Wahutu na watu wasiostahili, sio kutawala tu, bali hata kuishi Rwanda.

Ni ajabu mtu anaweza kuibuka tu na gazeti la aina hiyo na kuorodhesha kitu aliita amri kumi za Wahutu (vitu gani Mhutu anatakiwa kufanya ili kuwabagua kabisa Watutsi) likiwaweka watusi kuonekana kama ni maadui, watu wabaya na wasio waaminifu na liliwasema wanawake wa kitusi kuwa ni maajenti wa maadui waliokuwa msituni na kuwataka Wahutu kuchukua hatua dhidi Wanyarwanda wa Kitutsi waliokuwepo Rwanda kipindi hicho kwa kuwaaminisha watu kuwa hawana tofauti na wale walioko msituni. Mojawao ya maandishi liliandika: -

"tutumie njia gani kuwateketeza watusi moja kwa moja?

[45] This was a radio station created by the RPF in Uganda to counter hatred poured by the RTLM in Kigali.
[46]Schabas, W.A. 2000. Hate Speech in Rwanda: The Road to Genocide. McGill Law Journal,

Likachorwa panga ambalo ndiyo yaliyokuja kutumiwa katika kuwaua watusi.

Gazeti la kangura pia liliorodhesha watu lililowaita "***inkotanyi***" na kuweka hadi namba zao za magari ili wasiweze kabisa kutoroka na magari yao. **Kauli mbiu** yake ilikuwa ni

> **"***the voice which seeks to awaken and defend the majority people***" *(sauti inayowaamusha na kuwatetea walio wengi).***

Kama tulivyokwisha eleza hapo juu, gazeti hili liliungwa mkono/lilipata sapoti ya Serikali na viongozi wa serikali walilikika wakisema; - [47]

> *"**gazeti hili linatumia haki yake ya kutoa habari tu**".*

Kuanzia Aprili 1991 gazeti hili lilichapishwa bure na kampuni ya kupiga chapa ya Serikali [48]**.** Gazeti hili lilipata sapoti ya serikali kutokana na yale yaliyoandikwa.[49]

Katika hukumu ya kesi yao ya wanahabari iliyochukua takribani miaka mitatu, majaji wa Mahakama ya ICTR walimpata ***Hassan Ngeze***, ***Nahimana***, na ***Barayagwiza*** na Makosa wakisisitiza kuwa;

> **"*bila kutumia bunduki, panga au silaha yeyote inayoonekana mlisababisha vifo maelfu ya raia wasio na hatia".*** *Na kwamba walikuwa wanasambaza petrol nchini kidogo kidogo ili siku moja iweze kuwa rahisi kuwasha moto nchi nzima"***.**[50]

Georges Ruggiu.

Huyu alikuwa ni raia wa Ubelgiji aliyekuwa akifanya kazi kama mtangazaji wa redio ya **RTLM** kuanzia Januari 6, 1994 hadi Julai 14, 1994 [51]. Alishitakiwa Mahakama ya **ICTR** ambapo mwanzoni alikana kosa lakini baadaye alikiri kosa na kufungwa miaka 12. **Georges Ruggiu** alikiri yeye mwenyewe mbele ya Mahakama kwamba watu wengi waliuawa Rwanda na anaona kuna

---

[47]Kangura was joined by other newspapers that also received support from persons linked to the regime. Often, the written word was underscored by cartoons, most of them so graphic that they could not be misinterpreted (Des Forges 1999:67). For further reading about these cartoons, see Barcott, Rye (1999): Fear and Hate, Evocations of Genocide.

[48]Alexis and Mpambara 2003 at.15

[49] Kangura was joined by other newspapers that also received support from persons linked to the regime. Often, the written word was underscored by cartoons, most of them so graphic that they could not be misinterpreted (Des Forges 1999:67). For further reading about these cartoons, see Barcott, Rye (1999): Fear and Hate, Evocations of Genocide.

[50]The Prosecutor v. Ferdinand Nahimana, Jean- Bosco Barayagwiza, Hassan Ngeze, Case No. ICTR-99- 52-T, Judgement and Sentence, December 3, 2003.

[51]Prosecutor v. Ruggiu, Case No. ICTR 97-32-1, Judgment, 43 (June 1, 2000).

muunganiko wa moja kwa moja wa yale aliyoyasema yalichangia mauaji hayo na kwamba anajiona ana makosa.[52]

Uhusika wa wanamuziki

Wanamuziki au muziki ni vitu vyenye umaarufu vinavyoweza kufikisha ujumbe haraka na kwa kundi kubwa la watu, ambapo kama hawatatumiwa vyema wanaweza kuleta matatizo kwenye nchi. Hata hivyo, sio vibaya kuwatumia kwenye kampeni mbalimbali za uchaguzi au zinazohusu afya au mambo mbalimbali yanye kufikisha ujumbe kwa jamii. Jambo la kuelewa ni kwamba, yatokeapo matatizo kwa njia ya muziki, mwanamuziki husika ndiye wa kushughulikiwa, pamoja na wengine kama wapo.

Mwanamuziki SIMON BIKINDI

Wakati wa mauaji ya kimbari Rwanda, kwa mujibu wa Mahakama ya Kimataifa ya Rwanda (**ICTR**) mwanamuziki anayeitwa **SIMON BIKINDI** alizitumia shughuli zake za muziki kusambaza chuki na kugawa raia. **Simon Bikindi**, alizaliwa Rwanda tarehe **28/09/1954** eneo la ***Rwerere ya Gisenyi***, na mwaka 1994 alikuwa mwanamuziki maarufu pia akifanya kazi Wizara ya vijana na pia akiwa kiongozi wa kikundi cha muziki cha **IRINDIRO**[53]. Baada ya kuwa maarufu kutokana na muziki wake, wakati wa mauaji ya Kimbari 1994 alitumiwa na **INTALAHAMWE** kama nyenzo mojawapo ya kukusanya raia na ili kuwahutubia chuki dhidi ya Watusi.

Kwa umaarufu wake, alikuwa anazunguka na gari yenye kipaza sauti katika barabara ya Kivumu na Kayove akiimba nyimbo zake na watu wakikusanyika kumsikiliza hotuba za chuki zilitolewa. Baada ya mauaji ya Kimbari kutokea na Serikali mpya kuchukua madaraka Rwanda, alitorokea nchi za nje hadi alipokamatwa Uholanzi **tarehe 12/07/2001** akapelekwa kushitakiwa ICTR Arusha Tanzania. Miongoni mwa Makosa aliyoshitakiwa ambayo wanamuziki na wananchi wa kawaida wanatakiwa kuchukua kama fundisho ni "**public incitement to genocide (kosa la 4)** – yaani *kusambaza/kuhamasisha chuki ili kutekeleza kosa la kimbari*. Katika mashitaka hayo, pamoja na mengine aliyoshitakiwa, alikutwa na kosa la **kuhamasisha na kusambaza chuki kwa raia** na alipewa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 15 jela. [54].

Mahakama ya ICTR ilitambua pia kwamba zilikuwepo nyimbo zake nyingine alizokuwa ametunga kitambo kabla ya mauaji ya kimbari 1994, ambazo pia zilitungwa ili kupotosha historia ya Rwanda kwa nia ya kuwaunganisha wahutu dhidi ya watusi. Baadhi ya nyimbo hizo ni "**NANGA ABAHUTU**" na "**BENE SEBAHINZI**" ambazo ziliwaelezea wahutu kama ni ***watumwa wa Watusi***, na kwamba watusi ni maadui na marafiki wa maadui wa Rwanda.

---

[52] Ibid 53-55 (describing Ruggiu's guilty plea).

[53]The Prosecutor v. Simon Bikindi, Case No. ICTR-01-72-T Judgement and Sentence para.1-10 (2 December 2008).

[54]The Prosecutor v. Simon Bikindi, Case No. ICTR-01-72-T Judgement and Sentence para. 16

Nyimbo zake pia ziliwalaumu watusi kwa matatizo ya Rwanda zikiwataka wahutu waungane dhidi ya adui yao huyo mmoja. Vilevile alihamasisha amri kumi za wahutu zilizokuwa zimeorodheshwa kwenye **gazeti la Kangura**. Pamoja na kwamba ushahidi haukuimarisha "**nia" ya Bikindi kutunga nyimbo ambazo nyingine zilitungwa mwaka 1987**, kitu cha muhimu ambacho Mahakama ilisema ni kwamba **Simon Bikindi** alitunga nyimbo za **Nanga Abahutu** na **Bene Sebahinzi** akiwa na nia ya kuhamasisha propaganda za wahutu kuwachukia watusi.[55]

Pamoja na haya, Mahakama haikumkuta na ushahidi wa kutosha kuwa nyimbo zake hizo za zamani zilisababisha usambazaji wa chuki wa moja kwa moja uliosababisha mauaji mwaka 1994. Hii ina maana kwamba, kama mauaji yangetokea miaka aliyotunga nyimbo hizo angekamatika na kosa tu.

Uhamasishaji wake uliokuwa na ushahidi mzito zaidi na uliomtia hatiani ni ule aliotoa hotuba akiwa kwenye msafara na **interahamwe** barabara kati ya **KIVUMU** na **KAYOVE** alipotangaza kuwa wahutu wainuke kuwateketeza watusi walioko Rwanda. Baada ya kuimba nyimbo na raia wakakusanyika, aliwasalimia kwa kuwaambia: -

"*mmeshaua watusi hapa*?"

Akiwa na maana ya kutaka kuwapongeza wale ambao tayari wameshaua, na kuwahamasisha wengine ambao bado waende wakaue Watutsi. Tunaona hapa kumbe hata wanamuziki wanaweza kutumia umaarufu wao kuleta matatizo katika nchi. Mtu yeyote maarufu kama umaarufu wake hatautumia kwa uangalifu anaweza kuleta madhara katika jamii.

Uhusika wa Makanisa

Tukichukua mfano wa yaliyotokea nchini Rwanda mwaka 1994, mauaji yalipokuwa yanaendelea watusi wengi walikimbilia makanisani wakiamini wauaji hawawezi kuwaua wakiwa kanisani. Baadhi ya viongozi wa dini walikuwa wanawasilana na Intalahamwe wakitoa taarifa kuwa Watutsi wamekimbilia kanisani mwao. Mfano wake ni **Padre Athanase Seromba** ambaye kwa sasa anatumikia kifungo cha maisha baada ya kukutwa na hatia Mahakama ya ICTR Arusha. ***Seromba*** alikuwa Kasisi wa kanisa la Katoliki Parishi ya Nyange Mkoa wa Kibuye Rwanda Magharibi na alishitakiwa kusababisha vifo vya Watusi kama 2000 waliokimbilia katika kanisa alililoliongoza.

Mashitaka yalionyesha kwamba kati ya **April 6 na 20, 1994**, alielekeza kanisa lake livunjwe kwa katapila/bulldoza wakati raia wengi walikuwa ndani yake na wale waliojaribu kutoroka kujiokoa aliwapiga risasi. Mfano mwingine wa kasisi pia ni ***Padre Emmanuel Rukundo***.

[55]Ibid para 52-53

Mauaji mengine yaliyohusishwa kanisani ni ya Mwanasiasa maarufu aliyeitwa ***Eliézer Niyitegeka***; huyu pia alishitakia Mahakama ya **ICTR**[56] Kwa kuhamasisha Wahutu kuwaua watusi waliokuwa wamekimbilia kanisani. Katika kipaza sauti alisikika akiliambia kundi la watu 5,000 akiwashukuru kwa "***kazi nzuri***". Mahakama ilipata ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa matamshi ya neno "***kazi nzuri***" kwa raia ulikuwa msamiati wa kimafumbo ukimaanisha kazi ya kuwauwa Watutsi waliokimbilia kanisani mapema siku hiyo. Ilisemekana kwa kauli hizo alihamasisha mauaji mengine siku iliyofuata ambapo Watusi waliuawa eneo la ***Bisesero***.[57]Alipatikana na hatia na kufungwa kifungo cha maisha jela.[58]Bila kusahau **Mchungaji Elizaphan Ntakirutimana** aliyetuhumiwa kuwaongoza wauaji hadi Mugonero Complex walipokuwa wamejihifadhi kwa usalama raia wa kabila la Watutsi, wengi waliuawa. Alifungwa miaka 10 na ICTR.

Viongozi wanaweza kuwajibishwa kwa walio chini yao!

Katika Sheria za jinai ya Kimataifa, mwenye mamlaka anaweza kuwajibishwa kwa kosa wale wanaopokea amri toka kama mwenye mamlaka huyo alizembea walio chini yake wasifanye kosa, au alijua kosa linatendeka lakini hakufanya jitihada za kulisitisha au alijua tayari limeshatendeka lakini hakuchukua hatua kuwaadibisha wakosaji hao ambao wapo chini yake. Mfano wake ni kamanda wa kikosi cha jeshi, kamanda wa jeshi la polisi, Rais wa nchi, kiongozi wa kikundi cha uasi, au mtu yeyote alimradi tu awe na mamlaka na uwezo kuwathibiti au kuwaelekeza wengine wanaoonekana wamefanya tukio linaloangukia kwenye Mahakama ya ICC.

Kuwajibika kwa wenye amri au mamlaka kwa makosa ya wafuasi walio chini yao

Kisheria, Makamanda wa jeshi au wa kikundi cha wapiganaji anaweza kuwajibishwa kwa makosa ya wafuasi wake ambao anayo mamlaka kuwadhibiti, kusitisha kosa au kuwaadhibu wakikosea, na hajafanya hivyo, pamoa na kuwa na amri juu yao. Ibara ya 28 ya Sheria ya ICC inaeleza kwamba,

(a) Kamanda wa jeshi au mtu mwenye mamlaka kusimama kama kamanda wa jeshi atawajibika kwa makosa ya walioko chini yake ambao anayo mamlaka ya amri na ya kuwadhibiti, kama atakuwa amezembea kimamlaka kuwadhibiti (NB: ameshindwa kuwadhibiti kwa kuwazuia wasitende kosa, wanaendelea kutenda na hajawasitisha au wameshatenda na hajawaadibisha).

   (i) Kwamba kamanda au mtu huyo mwenye mamlaka/amri alijua, au mazingira yanaonyesha alitakiwa kujua au awe amejua kuwa

[56]Prosecutor v. Niyitegeka, Case No. ICTR 96-14-T, Judgment and Sentence (May 16, 2003).

[57] ibid

[58] Ibid para 480

wapiganaji wake walikuwa wanafanya kosa au walikuwa wanakaribia kutenda kosa, na,

(ii) Kamanda huyo wa jeshi au mtu mwenye mamlaka ya kijeshi juu yaw engine alishindwa kuchukua hatua za msingi ndani ya uwezo wake kuzuia, kusitisha uhalifu kuwapeleka wahalifu waliofanya makosa wakiwa chini yake, kwenye vyombo vyenye mamlaka ya kupeleleza na kuendesha mashitaka.

(b) Katika uhusiano wa mwenye mamlaka na mfuasi kama ilivyoelezwa katika aya ya (a), mwenye mamlaka atawajibika kwa makosa ya walioko chini yake kutokana na kushindwa kuwadhibiti, ambapo: -

(i) Mwenye mamlaka alijua au kwa makusudi alidharau taarifa iliyomfikia mapema kwamba watu wake wa chini walikuwa wanafanya uhalifu au walikuwa wanakaribia kufanya uhalifu.

(ii) Kosa lilihusisha shughuli zilizokuwa chini ya udhibiti na utawala wa mwenye mamlaka huyo.

(iii) Mwenye mamlaka huyo ameshindwa kuchukua hatua muhimu na za kueleweka ndani ya uwezo wake kuzuia, kusitisha uhalifu au kukabidhi suala hilo kwenye vyombo halali vya kiupelelezi na mashitaka.

Ibara ya 33 ya Sheria ya ICC inaeleza kwamba: -

(1) Hoja kwamba kosa limefanywa na mhalifu kwa amri ya Serikali au wenye mamlaka haitamwondolea mkosaji kuwajibika binafsi kwa kosa hilo, labda;

(a) Mhalifu alikuwa chini ya mamlaka ya kisheria kutii amri za Serikali au za Mwenye mamlaka juu yake (kwa maana kwamba kama asingetii angekuwa ametenda kosa la jinai kwa mujibu wa sheria zinazomtawala).

(b) Mtu huyo hakujua kama amri hiyo ilikuwa kinyume na sheria.

(c) Amri hiyo haikuwa kinyume na sheria waziwazi (ujinai ulijificha).

(2) Kwa malengo ya ibara hii, amri (za Serikali au wenye mamlaka) kutenda kosa la Kimbari au Uhalifu dhidi ya ubinadamu ni makosa ya waziwazi (yenyewe kama yalivyo ni makosa ya wazi hivyo afanyaye hawezi kujitetea kuwa hakujua kama amri ya kufanya hayo haikuwa ya waziwazi).

Kamanda au kiongozi afanye nini ili asishitakiwe the ICC?

Kwa kawaida kamanda wa jeshi au mtu yeyote mwenye mamlaka ya kijeshi dhidi yaw engine (hata kama ni raia mwenye wafuasi na nafasi kama hiyo), akitaka apone mkono wa Sheria, pindi tu akiona kosa linataka kutendeka azuie, likiwa limeshaanza

kutokea afanye jitihada kusitisha, na kama litakuwa limeshatendeka basi lazima awawajibishe kwa njia ya aidha kufuata vyombo vya sheria au kumkabidhi kwenye mamlaka halali ili awajibishwe kwa muujibu wa sheria.

Vyombo vya Habari Tanzania vinajifunza nini?

Tumeshashuhudia hapa Tanzania baadhi ya vyombo vya habari kama vile Radio na magazeti vikifungiwa kwa muda kama adhabu ya kusambaza chuki miongoni mwa raia au kukiuka maadili fulani ya Sheria za utangazaji. Mwaka 2013 ***Radio Iman*** ya Morogoro na ***Kwa neema radio FM*** ya Mwanza zilifungiwa kwa miezi sita. Gazeti la ***Mwanahalisi*** na mengine yalishafungiwa mara kadhaa. Sinyooshei kidole vyombo hivyo au nikithibitisha kwamba vilihusika au kutohusika na walichoadhibiwa nacho au pengine kama njia sahihi za uwajibishaji zilifuatwa kwa haki ama la;(hilo lipo mikononi mwa vyombo vilivyowajibisha), lakini tulichohushudia hasa kwa hizo radio ni kufungiwa kwasababu ya matangazo yaliyokiuka maadili, hasa kwenye kipengele cha chuki.

Popote palipo na uhuru wa habari, ijulikane kwamba hakuna uhuru usio na mipaka, na pale haki ya uhuru wako inapoishia, haki ya mwingine inaanzia (haki yako inaishia pale haki ya mwingine inapoanzia) hivyo uhuru usitumike kusababisha matatizo kwa wengine hasa kwenye nchi wanayoishi watu mchanganyik panapotakiwa watu kuishi kwa kuvumiliana na kuheshimiana. Kwa maslahi ya nchi, pamoja na kutakiwa kutoa uhuru wa habari nchini, Serikali inatakiwa kutumia sheria zilizopo kudhibiti kuenea kwa chuki za kidini, kisiasa na kikabila wakati wote.

MACHAFUKO YA NCHI YA LEBANON

Lebanon ni mfano hai wa nchi iliyokuwa ikiishi kwa amani na mshikamano raia wake wakiwa ni Wakristo kwa Waislam bila kubaguana kidini. Lakini baada ya kutokea Mauaji ya **Rafik Harrir** na kuingia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe (Wakristo dhidi ya Waislam) nchi ilisambaratika na mpaka leo inaishi na hali tete. Enzi hizo Lebanon ndio ilikuwa ikiitwa "***Paris of the Middle east***" sehemu ambayo ilikuwa mbali sana kiuchumi. Mabenki na taasisi za kifedha Lebanon ilikuwa mfano kwa Mashariki ya kati.

Lakini tofauti za kidini zilipoibuka, waliuana wao kwa wao na hadi sasa wengi wamesambaa dunia nzima kama wakimbizi. Laiti kama Walebanon wangepewa nafasi kurudi wawe kama walivyoishi zamani kabla ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, kila mmoja angekuwa balozi wa kuhubiri amani na mshikamano bila kujali tofauti ya dini na kuwapinga wote waliosababisha yote yale kutokea. Ilikuwa sawa na Tanzania yenye Waislam na Wakristo wengi pamoja lakini tunaishi kwa Amani na kwa ushirikiano bila kujali tofauti za dini zetu.

JAMHURI YA AFRIKA YA KATI NA NIGERIA KASKAZINI

Nchi hizo pia zimekaliwa na watu wengi wenye Imani tofauti ambao awali walikuwa wakiishi pamoja wakishirikiana wakiheshimiana. Lakini dunia imeshuhudia machafuko ya kidini (Wakristo dhidi ya Waislam) katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, na vikundi vya ugaidi Nigeria ya kaskazini. Watu wa nchi moja wanauana wao kwa

wao kwasababu ya tofauti tu za dini, matokeo yake wote wanapata adha za vita, wanakufa au wanaharibu mfumo wote wa uchumi wa nchi.

Kinachotakiwa kwa nchi kama Tanzania na nchi nyingine za Afrika ni kujifunza madhara ya kiuchumi na kijamii yanayotokana na chuki za kidini ambavyo hupelekea vita vya kidini, ili kwa kutumia sheria viashiria vyote vizimwe kabla havijaleta madhara. ***Rais Jakaya Mrisho Kikwete*** alishawahi kusema kuwa "***vita vya kidini havina mshindi, sisi sote kama tutagombana kwasababu ya tofauti zetu za kidini hakuna atakayeshinda, sisi sote tutakuwa washindwa***".

HALI HALISI ILIVYO HIVI SASA HAPA TANZANIA

- ✓ Kwa sasa, Tanzania ni nchi ya mfano wa kuigwa kwa nchi nyingi duniani, kwanza kuwa muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar ambao umedumu, wakati miungano mingine ilivunjika (mfano; Senegal na Ghamia-Senegambia n.k), pia idadi kubwa ya Wakristo na Waislam kuishi pamoja kwa Amani bila kujali tofauti za dini, na jingine kubwa zaidi, uwepo wa makabila zaidi ya 120 yenye lugha tofautitofauti lakini Watanzania hatujagawanyika kikabila. Tunaoleana na hata katika chaguzi za uongozi mtu wa kabila hili anaweza kuacha mgombea wa kabila lake akapigia kura mgombea wa kabila jingine n.k. hilo ni jambo ambalo nchi nyingi hazijabahatika kuwa nalo, na Watanzania wote kwa pamoja tunatakiwa kulithamini na kulilinda. Akitokea yeyote anayetaka kututenganisha yatupasa sote kwa pamoja kuungana kumpinga.

- ✓ Hata hivyo zipo changamoto kadhaa zinazotakiwa kuendewa kwa busara na hekima. Mfano; wakati wa kampeni za kisiasa au wakati wa kawaida, yanaweza kuwepo maandamano mbalimbali, mengine yenye Baraka/kibali za Serikali au yasiyo na kibali. Wajibu upo pande zote mbili, Serikali na Wanasiasa kwamba kama kutahitajika kuzuia maandamano, sheria za jinai za kimataifa zinakataza nguvu kupika kiasi kutumika kwa raia ambao hawaleti hatari au wasio na silaha. Vilevile, kwenye mikutano ya hadhara au uhamasishaji maandamano, viongozi watambue kuwa watawajibika kwa kila wanachohubiri kama kitaleta madhara.

- ✓ Watanzania wengine wameshauri kwamba, vikundi vya mgambo vya vyama mbalimbali havileti afya katika jamii. Kwa Tanzania tunazo "Red Brigade za CHADEMA na "Green Guards" za CCM. Kama jeshi la Polisi lenye wajibu wa kulinda raia na mali zao lipo na uwepo wake umetungiwa sheria, hivi vikundi binafsi vya chama kazi yao ni nini, na ni sheria gani ya nchi inaviongoza ili visivunje sheria? Wananchi wengine wanafananisha vikundi hivi na wanamgambo wa ***Intalahamwe*** Rwanda 1994, na waliruhusiwa na Serikali ya kipindi hicho.

- ✓ Wanamuziki mbalimbali wanatumika kwenye kampeni za chaguzi mbalimbali, kwasababu wao ni maarufu wajitahidi wasitumiwe kama nyenzo kusambaza chuki dhidi ya makundi tofauti tofauti.

- ✓ Kuna wakati mwingine baadhi ya wahubiri wa Imani tofautitofauti **MAASKOFU, WACHUNGAJI, MAPADRI, MASHEHE NA MAIMAM** wamekuwa na ndimi zinazoteleza hata kusambaza chuki dhidi ya Serikali au Imani nyingine tofauti na zao. Ni vigumu kufumba macho na kusema nchini kwetu tumekuwa watakatifu asilimia mia moja, kwasababu ni muhimu palipo na nyufa tuzibe

kabla hapajasambaa. Kama viongozi wa dini Rwanda walivyokuwa madhabahuni na wakati huohuo wakiwa na ukabila mioyoni, ndivyo wengi wanavyoweza kuwa madhabahuni kwenye nchi zetu na wakati huo huo wakawa wadini na wakabila kupindukia mioyoni.

- ✓ Viongozi wa serikali na Makamanda wa Majeshi ni lazima kuzuia, kusitisha au kuwajibisha walioko chini yao kama watafanya makosa yanayodondokea kwenye Mahakama ya ICC, ama la, wao watawajibika pamoja nao. Hii sio lazima itokee wakati au maeneo ya vita, kwasababu kuna makosa katika Mahakama ya ICC yanayotikea wakati wa Amani. Mfano, vyombo vya dola vikikabiliana na raia wasio na silaha kuna uwezekano mkubwa uhalifu dhidi ya ubinadamu yakatendeka, hivyo wakuu wa majeshi kabla watu wao hawajatumwa au wakiwa pamoja nao huko kwenye mapambano dhidi ya raia wasio na silaha, yawapasa kuwadhibiti, kuwasitisha au kuwawajibisha watakaotenda makosa.

Yapo mengi ambayo tungeongelea hapa,

Tanzania tumejifunza nini kwa uchaguzi Kenya 2007/2008 na machafuko nchi zingine?

(1) Tanzania tumejifunza nini kutokana na machafuko ya kisiasa yaliyotokea wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2007/2008 Kenya? Tukienda moja kwa moja bila kupepesa macho, tumejifunza kwamba machafuko yeyote yakitokea viongozi waliohamasisha au kuzembea, au kuongoza wengine kufanya uhalifu ndio watakaoshughulikiwa na Mahakama ya ICC.

(2) Pia tumejifunza kwamba, Mahakama ya ICC haiingilii moja kwa moja kwenye nchi zetu kupeleleza na kushitaki mtu; nafasi ya kwanza kushughulikia wahalifu ipo mikononi mwa nchi husika wenyewe ila ikiwa haina nia kushughulikia, ikiwa haina uwezo au ikishughulikia kama gelesha, Mahakama ya ICC itaingilia kati.

(3) Vilevile, Mahakama ya ICC inashughulikia watu wote bila kujali cheo/wadhifa; tulishuhudia Waandishi wa habari, Makamu wa Rais Mh. Ruto pamoja na Raisi Uhuru Kenyatta wakisafiri hadi Hague Uholanzi kila wakati wa kesi, bila kujali nyadhifa kubwa sana walizonazo. Rais wa zamani wa Sudan Al Bashir alishawahi kufunguliwa Mashitaka Mahakama ya ICC pia akituhumiwa na mauaji ya kimbari ya waafrica weusi katika jimbo la Darfu wakati bado akiwa madarakani (***ibara ya 27 ya sheria ya ICC***).

(4) Yapo mataifa yaliyoishi kwa Amani bila kujali tofauti za kidini au zakikabila kama ilivyo Tanzania, lakini usambazaji wa chuki uliwagawanya wananchi hadi wakaingia kwenye machafuko na matokeo yake watu wao wamekuwa wakimbizi waliosambaa dunia nzima. Mfano; Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Rwanda ya zamani (sio hii ya sasa, kwa sasa Rwanda imebadilia na kuwa mfano wa kuigwa), Burundi, Bosnia katika Yugoslavia ya zamani, Somalia n.k.

(5) Tumejifunza pia kuwa, vyombo vya habari ni nyenzo muhimu kusambaza amani na mshikamano lakini watu wenye nia mbaya wanaweza kuvitumia kusambaza chuki na upotoshaji kwenye jamii. Na pia wananchi wa kawaida wanaamini kiurahisi sana kitu wanachoona au kusikia toka kwenye vyombo vya habari, hivyo

ni lazima vidhibitiwe kwa mujibu wa sheria, bila kuathiri matakwa ya uhuru wa habari na haki ya kupata habari kwa wananchi. Maslahi ya nchi yatangulie.

Dunia imekuwa kijiji

Kutokana na mitandao ya kijamii pamoja na vyombo vya habari, jambo lolote baya au zuri likitokea sehemu moja ya nchi laweza kusambazwa dunia nzima saa na siku hiyohiyo. Hii ina faida na hasara kwasababu pamoja na kusambaza mambo mema, hata uzushi unaoweza kulichafua taifa waweza kuenea haraka na kwa watu wengi kiasi hicho. Pia, jambo jingine la faida ni kwamba, uhalifu ukitendeka nchi moja taarifa zake zaweza kuenea dunia nzima muda mfupi hivyo kufanya mhalifu asiwajibike tu kwa nchi yake bali kwa dunia nzima.

Hii maana yake, kama nchi husika haitawajibisha wahalifu, uhalifu huo umeshajulikana na kumbukumbu zake kuhifadhiwa dunia nzima hivyo Mahakama hii ya ICC inaweza kumwajibisha mtuhumiwa kwasababu nchi husika haitafanya hivyo. Mfano wake ni maandamano katika nchi za kiarabu Video mbalimbali zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii na dunia nzima iliona kilichokuwa kinaendelea n.k, pia kwenye matukio ya vita zinazoendelea dunia nzima inapata picha ya kinachoendelea kwenye uwanja wa vita; hii ni muhimu kwasababu watuhumiwa wanahukumia sio na watu wa nchini kwake tu bali na dunia nzima hivyo hana pa kujificha. Video hizo zinaweza kutumika kama ushahidi vilevile hii ndio sababu busara yapaswa kutumika katika kila jambo tunalolifanya.

VIKUNDI VYA ULINZI KATIKA VYAMA VYA SIASA TANZANIA

Hapa Tanzania kuna vikundi vya ulinzi mfano wa askari mgambo ambavyo baadhi ya vyama vya siasa wameviunda. Vinasemekana kutumika pia kulinda kura wakati wa uchaguzi au kulinda baadhi ya maslahi ya chama hasa kwenye mikutano ya hadhara n.k. kwa maoni yangu, vikundi hivi yawezekana havijaundwa kwa nia mbaya au kutumika vibaya, lakini binafsi nisingeshauri viwepo kabisa hapa Tanzania kutokana na yale tunayojifunza toka Rwanda.

Rwanda kulikuwa na wanamgambo wa aina hiyo walioitwa **INTERAHAMWE**. Kikundi hiki kilitumika sana katika mauaji ya kimbari Rwanda kwa kuwasaka raia majumbani mwao na wengine kuzuiliwa kwenye vizuizi vilivyokuwa vimesambaa barabarani kuchunguza nani mtusi na nani sio mtusi kwa njia ya vitambulisho vilivyokuwa vimeainisha kabla na muonekano wa sura pia. Tunaishukuru serikali ya Tanzania kwa kutoweka kipengele cha dini katika passport zetu au vitambulisho vya uraia. Kwa minajiri hiyo, ni bora vyombo vya ulinzi vinavyotambulika vikatumika katika ulinzi kuliko vikundi hivi visivyo rasmi ambavyo wakati mwingine vinaweza kusababisha vurugu. Kama polisi wapo, wanajeshi, usalama wa taifa, uhamiaji n.k wapo, red brigade na green brigade wana umuhimu gani katika nchi?

HITIMISHO

Kitabu hiki kimesambazwa bure kwenye mitandao, na mwandishi anatarajia wasomaji watapata uelewa wa umuhimu au kutokuwa na umuhimu kwa Mahakama ya Kimataifa ya jinai (ICC) kwetu sisi Watanzania kama wanachama wa Mkataba wa Roma wa Mahakama hiyo. Mara nyingi watu wamekuwa wahihusisha Mahakama hii na makosa ambayo hata haiyapokei, na pia kitabu hiki kiwe kama ukumbusho kwa vingozi mbalimbali wa kisiasa, kidini n.k kuzuia makosa yasitendeke kwasababu yakitendeka wahusika watawajibishwa. Asante.

KUMBUKA: **usikoke kupata nakaza muhimu za vitabu vilivyoandikwa na Ofmedy Mussa Mtenga**, ni mwenendo mzuri sana wa hatua kwa hatua uendeshaji kesi Mahakama za Wilaya na Mkoa, na kingine ni hatua kwa hatua uendeshaji kesi Mahakama Kuu. Ndani yake kuna kesi mpya hadi zilizoishia 2019 na ni maalumu kwa "practice". Nawashukuru Waheshimiwa Majaji na Waheshimiwa Mahakimu, Mawakili wa Kujitegemea na Mawakili wa Serikali kwa kunitia moyo kwa kuvisifia sana vitabu hivi, kwasababu vimekuwa msaada mkubwa katika uandeshaji kesi. Principles zilizoko ndani yake zinasaidia pia kwa wale wanaoendesha kesi Mahakama ya Rufaa. Sifa, Shukrani na Utukufu wote ni kwa Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango kwenye tasnia ya sheria.

(1) *CRIMINAL PRACTICE MANUAL, a step by step guide to Trials in* ***Subordinate Courts***

(2) *CRIMINAL PRACTICE MANUAL , A best Practice Guide to Trials in the* ***High Court***

(3) *Appeals and Applications before the* ***Court of Appeal*** *(kinachoongelea aplications, appeals, Review na References).*

Wasiliana nasi: ***0767154141***

JIFUNZE SHERIA
LAW BOOKS & CASE LAWS

MAREJEO

ORODHA YA SHERIA ZILIZOTUMIKA

(1) Additional Protocol I to the Geneva Conventions (AP I)

(2) Common Art. 3 to the Geneva Conventions

(3) Geneva Conventions 1949 (adopted 12 Aug. 1949, entered into force 21 Oct. 1950) (GC I-IV),

(4) Mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN Charter)

(5) The Statute of the International Criminal Court of Justice (ICJ Statute)

(6) The Rome Statute of International Criminal Court (ICC Statute)

ORODHA YA VITABU NA MAKALA ZILIZOTUMIKA

(1) Alexis and Mpambara 2003 at.15

(2) Alison des Forges, (1999) "Leave none to tell the story": Genocide in Rwanda at 72.

(3) Allan Thompson ed., 2007

(4) Barcott, Rye (1999): Fear and Hate, Evocations of Genocide.

(5) Christine L. Kellow & H. Leslie Steeves, The Role of Radio in the Rwandan Genocide, J. COMM., Summer 1998, at 107, 123

(6) **ICC Elements of Crime** (unaweza kuipakua toka kwenye mtandao bure).

(7) International Convention for the Protection of All Persons from Enforced Disappearance

(8) Jean-Marie Vianney Higiro, Rwandan Private Print Media on the Eve of the Genocide, in The media and the Rwanda Genocide 73, 84

(9) Kirschke, Linda (1996): Broadcasting Genocide: Censorship, Propaganda & State-Sponsored Violence in Rwanda 1990-1994, ARTICLE 19, London.:47, 70-71

(10) Office of the United Nations High Commissioner for Human Rights, Enforced or Involuntary Disappearances, act Sheet No. 6/Rev.3 - pg.11

(11) Gérard Prunier,The Rwanda Crisis, 1954-1994: The History of a Genocide – Nov 30, 1995

(12) Schabas, W.A. 2000. Hate Speech in Rwanda: The Road to Genocide. McGill Law Journal

(13) Schabas, W.A., Genocide in International Law – The Crime of Crimes, Second edition, Cambridge: Cambridge University Press, 2009.

(14) Tharcisse Gatwa, Ethnic Conflict and the Media: The Case of Rwanda, 42 MEDIA DEV. 3, (1995).

ORODHA YA K ESI ZILIZOTUMIKA

(1) Aloys Simba, Case No. Ictr-01-76-A, Appeal Judgement, 27 Nov. 2007, 266;

(2) Blaškid, AJ 113 – 115; Mrkšid, AJ 35;

(3) Čelebidi, Trial Judgment 461-469; Furundžija, Appeal Judgment 113.

(4) Clément Kayishema et al., Case No. ICTR-95-I-A, Appeal Judgement, 1 June 2001, 91.

(5) Dragoljub Kunarac et al., Case No. IT-96-23-A, Appeal Judgement, 12 June 2002, 86.

(6) Duško Tadid, Case No. IT-94-1-T, Trial Judgement, 7 May 1997, 644.

(7) Gacumbitsi, AJ 147-157. ICC Elements of Crimes, Art. 7(1)(g)-1(1), Art. 7(1)(g)-2(2).

(8) Georges A. N. Rutaganda, Case No. ICTR-96-3-T, Trial Judgement, 6 Dec. 1999, 59.

(9) Jean-Pierre Bemba Gombo, Pre-Trial Chamber II, 15 June 2009,78;
(10) Krnojelac, Trial Judgment, 326, na Brđanin, Trial Judgment 385
(11) Kunarac et al., AJ 91-2;
(12) Milomir Stakid, Case No. IT-97-24-T, Trial Judget, 31 July 2003, 624;
(13) Martid, AJ 313; Blagojevid et al., TJ, 544.
(14) Milan Milutinovid et al. ("Šainovid et al.".), Case No. IT-05-87-T, Trial Jdjt, 26 Feb. 2009, 194
(15) Mitar Vasiljevid, Case No. IT-98-32-T, Trial Judgement, 29 Nov. 2002, 33.
(16) Moinina Fofana et al. (CDF Case), Case No. SCSL-2003-11-T, Trial Judgemt, 2 Aug. 2007, 144
(17) Moinina Fofana et al., Case No. SCSL-2003-11-A, Appeal Judgement, 28 May 2008, 247,
(18) Mugesera v. Canada (Minister of Citizenship and Immigration), [2005] S.C.C. 40, 69, app. III 18.
(19) Prosecutor v Bagilishema, No. ICTR-95-1A-T (Trial Chamber), June 7, 2001. para. 80
(20) Prosecutor v Semanza, Case No. ICTR-97-20 (Trial Chamber), May 15, 2003. para 326.
(21) Prosecutor v Tadic, Case No. IT-94-1 (Appeals Chamber), Decision of the Defence Motion for Interlocutory Appeal on Jurisdiction, October 2, 1995, para. 70.119
(22) Prosecutor v. Akayesu, Case No. ICTR 96-4-T, Judgment (Sept. 2, 1998).
(23) Prosecutor v. Ferdinand Nahimana, et al, No. ICTR-99- 52-T, Jdg and Sentence, Dec 3, 2003.
(24) Prosecutor v. Jelisic, Case No. IT-95-10, 14 December 1999, para. 70.
(25) Prosecutor v. Kambanda, Case No. ICTR 97-23-S, Judgment, 39 (Sept. 4, 1998).
(26) Prosecutor v. Kayishema and Ruzindana, Case No. ICTR-95-1-T,21 May 1999, para. 98
(27) Prosecutor v. Kordic and Cerkez, Case No. IT-95-14/2 (Trial Chamber), Feb 26, 2001 para. 32.
(28) Prosecutor v. Niyitegeka, Case No. ICTR 96-14-T, Judgment and Sentence (May 16, 2003).
(29) Prosecutor v. Rutaganda, Case No. ICTR-96-3-T, Judgment, Trial Chamber, 6 Dec1999
(30) Prosecutor v. Simon Bikindi, Case No. ICTR-01-72-T Jdgt and Sentence para.1-10 (2 Dec. 2008).
(31) Radislav Krstid, Case No. IT-98-33-A, Trial Judgement, 2 Aug. 2001, 590 (ICTY);
(32) Radoslav Brđanin, Case No. IT-99-36-T, Trial Judgement, 1 "
(33) Situation in the Republic of Kenya, 31 March 2010, 82 (fn 74),
(34) Stanislav Galid, Case No. IT-98-29-A, Appeal Judgement, 30 Nov. 2006, 136 – 137, fn 437;
(35) Tihomir Blaškid, Case No. IT-95-14-A, Appeal Judgement, 29 July 2004, 106
(36) Tihomir Blaškid, Case No. IT-95-14-T, Trial Judgement, 3 March 2000, 205.
(1) Vidoje Blagojevid et al., Case No. IT-02-60-T, Trial Judgement, 17 Jan. 2005, 544.

DRM Software Review